# Nipashe

Jumamosi Mei 2, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580221

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

...ian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




## Dk. Reginald Mengi: 'His Legacy lives on'

UKURASA 3




UKURASA 11

MEI MOSI

# JPM: Corona isiwe sababu wafanyakazi kunyanyaswa



• **Asisitiza** atasimamia maslahi yao, agusia baa la corona... Uk.2



### BAA LA CORONA

**Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), visa vilivyoripotiwa hadi jana duniani vya maambukizo ya Covid- 19 ni 3,145,407, vifo 221,823 na nchi na maeneo yaliyoathiriwa 214.**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

TISHIO LA CORONA

## Wabunge Chadema wakimbia Bunge

UKURASA 2



Waziri wa Sheria na Katiba, Augustine Mahiga. **PICHA: MTANDAO**

## Rais Magufuli, mabalozi wamlilia Waziri Mahiga

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** **MAPUMZIKO CORONA YAINUFAISHA NDANDA** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# JPM: Corona isiwe sababu wafanyakazi kunyanyaswa

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amewataka waajiri wote wa serikali na sekta binafsi kutotumia mlipuko wa virusi vvya corona kama kigezo cha kuwanyanyasa wafanyakazi wao.

Rais alitoa rai hiyo jana kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, kuhusu maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi) ambayo kwa mwaka huu hayajafanyika nchini, ili kuepuka mikusanyiko ya watu kutokana na corona.

"Ninawapongeza waajiri wote wa serikali na sekta binafsi na ninatoa wito kwao kutotumia ugonjwa wa corona kama kigezo cha kuwanyanyasa wafanyakazi," aliagiza.

Rais Magufuli pia aliwapongeza na kuwatakia heri wafanyakazi wote ambao waliadhimisha siku yao.

"Mwaka huu sherehe hizi hazitafanyika kuepuka mikusanyiko ya watu, ikiwa ni hatua muhimu ya kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona," alisema.

Rais Magufuli alisema licha ya kwamba sherehe hizo hazijafanyika, serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na wafanyakazi katika ujenzi wa taifa.

Alisema serikali itaendelea kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kuboresha mazingira yao ya kazi.

Rais Magufuli aliwataka wafanyakazi kuendelea kuchapa kazi kwa juhudi na maarifa ili Watanzania waendelee kunufaika na huduma wanazozitoa katika maeneo yao ya kazi.

"Chukueni tahadhari zote zinazoelekezwa na wataalamu kuhusu kujikinga na ugonjwa wa corona. Ndugu wafanyakazi wenzangu, nawapongeza sana kwa kuchapa kazi.

"Nipo pamoja nanyi na natambua kazi nzuri mnayoifanya, nawaomba katika kipindi hiki ambacho dunia inapitia katika wakati mgumu wa kukabiliana na ugonjwa wa corona, tuendelee kuchapa kazi.

"Kamwe ugonjwa huu usiwe sababu ya kurudi nyuma na kuacha kuwahudumia Watanzania, ninaamini mwenyezi Mungu atatuvusha," Rais Magufuli alinukuliwa katika taarifa hiyo ya Ikulu.



Bodaboda wakiwavusha watu kutokana na barabara eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam, kujaa maji mchana na kufungwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## TISHIO LA CORONA

# Chadema walikimbia Bunge

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimewazuia wabunge wake kuhudhuria vikao vya Bunge kuanzia Jumatatu na kuwataka kujiweka karantini kwa siku 14 kutokana na tishio la virusi vya corona.

Vilevile, chama hicho kimewataka wabunge wake kutosafiri kwenda nje ya Dodoma, huku kikitaka Bunge kusitishwa na baadhi ya vikao muhimu kufanyika kwa mtandao.

Bunge la Bajeti linaloendelea jijini Dodoma, lilianza Machi 31 mwaka huu na lilitarajiwa kufika ukomo Juni 30 mwaka huu, siku ambayo pia Rais John Magufuli anatarajiwa kulifunga Bunge la 11.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe, ilibainisha hatua tano zilizofikiwa na chama hicho kuhusu wabunge wao na zitaanza kutekelezwa mara moja katika kikao cha keshokutwa.

Katika taarifa hiyo, Mbowe alisema maazimio hayo ni wabunge wa Chadema kuacha mara moja kuhudhuria vikao vya Bunge na kamati za Bunge.

Alisema uamuzi mwingine uliochukuliwa ni wabunge hao kutofika kabisa katika eneo lote la Bunge jijini Dodoma na ofisi za Bunge jijini Dar es Salaam.

Mbowe pia aliwataka wabunge wote kujiweka katika karantini kwa muda usiopungua wiki mbili.

"Tunasisitiza wabunge wetu walioko Dodoma wasiende majimboni, mikoani, bali wabaki Dodoma kwenye karantini hadi itakapothibitika wao ni salama na au kupata maelekezo mengine yoyote yaliyo rasmi," alisema.

Mbowe alisema ni vyema wabunge wa vyama vingine kutafakari kama kweli ni salama kuendelea na vikao vya Bunge katika mazingira yaliyopo.

"Tunalitaka Bunge kutisha shughuli za Bunge kwa siku 21 kuruhusu wabunge na watumishi wote wa Bunge kwenda karantini, kupima wabunge wote, watumishi wa Bunge na familia zao kubaini ni wangapi tayari wana maambukizo ya virusi, ili hatua stahiki za kitabibu ziweze kuchukuliwa," alishauri.

Mbowe pia alisema chama chao kinashauri kamati mahsusi za Bunge hususani kamati ya huduma za Bunge na kamati za uongozi, zifanye vikao vyake kwa njia ya mtandao ili uamuzi muhimu kuhusu utawala na mwenendo wa Bunge ufanyike.

Alisema Chadema inaendelea kusisitiza Watanzania wote kuwa mstari wa kwanza wa kinga, kila mmoja kujikinga badala ya kutegemea mtu mwingine.

Hivi karibuni Mbowe, alihutubia taifa kwa njia ya mtandao na kutaka hatua mbalimbali kuchukuliwa ikiwamo kufunga nchi kwa muda na kupima watu wengi.

Hadi sasa, Bunge la Bajeti

INAENDELEA UK. 19

# JPM, mabalozi, wabunge wamlilia Mahiga

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

RAIS John Magufuli, mabalozi na wabunge wameeleza namna walivyoumizwa na kifo cha Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Augustine Mahiga (75), aliyefariki jana alfajiri nyumbani kwake jijini Dodoma.

Jana asubuhi, Rais alitangaza kifo cha Mahiga ambaye alikuwa mbunge wa kuteuliwa, akibainisha kuwa kiongozi huyo aliugua ghafla nyumbani kwake na alifikishwa hospitalini akiwa tayari ameshafariki dunia.

Rais alitoa salamu za pole kwa familia, Spika wa Bunge, Job Ndugai, wabunge, wafanyakazi wa wizara yake na wananchi wa Mkoa wa Iringa kwa kuondokewa na mpendwa wao na kwamba anaungana nao katika kipindi hiki kigumu cha majonzi.

Kwa mujibu wa Rais Magufuli, Balozi Mahiga alikuwa mchapakazi, mwadilifu, mzalendo na mwanadiplomasia mahiri aliyeiwakilisha na kuipigania Tanzania katika nyanja za kimataifa kwa miaka mingi.

"Pamoja na umri wake mkubwa na uzoefu wa kushika madaraka katika nyadhifa mbalimbali za kitaifa na kimataifa, Balozi Mahiga alikuwa mnyenyekevu na mtiifu kwa kila jukumu nililomtuma,"Rais Magufuli alisema.

**MABALOZI WAMLILIA**

Mabalozi mbalimbali jana walitoa salamu za pole huku wakimwelezea Balozi Mahiga kwa uadilifu na weledi wake.

"Kwa huzuni kubwa nimepokea taarifa za kifo cha Mheshimiwa Mahiga, ambaye alikuwa mwenye hekima na mwanadiplomasia mzoefu, ambaye alikuwa rafiki yetu Uingereza. Ninaiombea familia yake katika kipindi hiki kigumu," alisema Balozi wa Uingereza nchini.

Balozi wa Sweden nchini, Anders Sjoberg, alisema: "Ni kwa masikitiko makubwa tumepokea taarifa za kifo cha Dk. Mahiga ambaye alikuwa mwanadiplomasia wa kutegemewa, mpiganiaji wa ukweli wa haki za binadamu na rafiki mkubwa wa Sweden. Salamu zangu za rambirambi ni kwa familia yake. Apumzike kwa amani."

Ubalozi wa Ufaransa ulisema jana kuwa: "Tanzania imepoteza mwanadiplomasia mkubwa, Mheshimiwa

INAENDELEA UK. 19



# Dr. Reginald Mengi

## His Legacy Lives On

IPP

Will Always Care For You

# Mwili wa Jaji Ramadhani waagwa, akumbukwa kwa uadilifu uliotukuka

**Na Beatrice Moses**

MWILI wa Jaji Mkuu mstaafu, Augustino Ramadhan, umeagwa jana katika viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam huku akitajwa kuwa mwadilifu na mwenye utumishi uliotukuka.

Mwili huo uliagwa kwa maombi kutoka kwa Askofu wa Kanisa la Anglikana, Dayosisi ya Dar es Salaam, Jackson Sosthenes na Sheikh Mkuu wa mkoa huo, Alhaji Mussa Salum kwa niaba ya Mufti wa Tanzania.

Jeneza lililohifadhi mwili wake lililoingizwa kwenye viwanja hivyo na maofisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), lilifunikwa kwa Bendera ya Taifa na juu kuwekwa joho maalum ambalo huvaliwa na majaji.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Mussa, katika hotuba yake alisema kutokana na utumishi wake uliotukuka, Jaji Ramadhan alikuwa akihitajika katika tasisi nyingi, aliazimwa kutoka JWTZ na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuwa Jaji Mkuu Msaidizi.

Profesa Mussa alisema enzi za uhai wake Jaji Ramadhani ametumikia kwa miaka 50 ya uanasheria na kuacha hazina kubwa ya uzoefu, alidumu Mahakama ya Rufani kwa miaka 21 na ilikuwa ni miaka ya kutoa maamuzi ya mwisho ya kimahakama ni majaji wachache wanajaliwa kupata nafasi hiyo.

Katika uhai wake, Jaji Ramadhani alikuwa akielezea kuumizwa na jinsi wananchi wengi wakiwamo waliosomea sheria ambavyo hawana kawaida ya kusoma hukumu bali wanasubiri majibu rahisi ya kesi nani ameshinda au ameshindwa, hatua inayowafanya wengi kushindwa kujua mapendekezo yanayotolewa na mahakama.

Alisema siku zote Jaji Ramadhan alikuwa na tabia ya kuwahimiza wanasheria na wananchi kusoma hukumu mbalimbali, akitoa mfano wa kesi iliyofunguliwa na hayati Mchungaji Christopher Mtikila ya mwaka 2009, licha ya kuelimisha ilimpambanua kama jaji aliyeheshimu mipaka ya migawanyo wa mamlaka kama ilivyowekwa na Katiba.

Profesa Mussa, alisema kesi hiyo ilisikilizwa na jopo la majaji saba ambao waliongozwa na Jaji Ramadhan na licha ya kutoa jibu, lakini walitoa jibu jinsi ambavyo Bunge linaweza kushiriki kwa kufuata kanuni zilizopo kufanya mabadiliko kwenye Katiba.

Kwa upande wake, Waziri wa Ulinzi, Hussein Mwinyi alisema, Jaji Ramadhani alikuwa na kipaji cha aina yake, kwa kuwa aliweza kumudu kazi alizokabidhiwa na SMZ na Serikali Kuu na kuzifanya kwa kiwango chenye mafanikio hivyo atakumbukwa daima.

Kutokana na kuepusha mambukizo ya virusi vya ugonjwa wa homa kali ya mapafu, Covid-19, shughuli ya kuagwa kwa mwili huo ilihudhuriwa na watu wachache wakiwamo baadhi ya viongozi wa serikali pamoja na Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamini Mkapa na aliyekuwa Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete.

Jaji Ramadhani ambaye alishiriki kwenye vita vya kumng'oa Nduli Idd Amin wa Uganda, ameacha mjane ambaye ni Luteni Kanali mstaafu, Sada Ramadhan pamoja na watoto wanne.

Alistaafu kwa hiyari JWTZ akiwa na cheo cha Brigedia Jenerali, Rais wa Mahakama ya Afrika, Makamu Mwenyekiti Tume ya Katiba, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu, 2013 alitawazwa kuwa mchungaji katika Kanisa la Anglikana, alikuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Iringa pia aliwahi kuwa mlezi wa chama cha mpira wa miguu.

# Wanufaika mamilioni mikopo halmashauri

**Na Tiganya Vincent, NZEGA**

HALMASHAURI ya Mji wa Nzega mkoani Tabora, imefanikiwa kutoa mikopo ya Sh. milioni 90 kwa vikundi mbalimbali kwa mwaka huu wa fedha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Philemon Magesa, aliyasema hayo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani.

Alisema Sh. milioni 40 zimetolewa kwa vikundi 26 vya wanawake, Sh. milioni 33.6 zimekopeshwa kwa vikundi 12 vya vijana na vikundi vinne vya watu wenye ulemavu vimekopeshwa Sh. milioni 16.

Hata hivyo, Magesa alibainisha kuwa, vikundi vya wanawake na walemavu vimekuwa warejeshaji wazuri kulinganisha na vikundi vya vijana.

Alisema hadi sasa kwa kutumia Kitengo cha Sheria, wanaendelea kuwafuatilia na kuwachukulia hatua wadaiwa wanaosumbua na kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Magesa aliongeza kuwa katika kufuatilia madeni, wamefanikiwa kurejesha Sh. milioni 17.7 ambapo kati yake, Sh. milioni 5.3 zimerejeshwa na vikundi vya vijana, Sh. milioni 9.3 zimerejeshwa na wanawake na Sh. milioni 3.1 zimerejeshwa na vikundi vya watu wenye ulemavu.

Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, aliipongeza Halmashauri ya Mji wa Nzega kwa kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa asilimia 100.

Aliutaka uongozi wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanawafuatilia wadaiwa ili kurejesha fedha walizokopeshwa ili kusaidia vikundi vingine.

Katika hatua nyingine, Halmashauri ya Mji wa Nzega imefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 1.2, sawa na asilimia 61 ya lengo la kukusanya Sh. bilioni mbili mwaka huu wa fedha.

Magesa alisema hadi mwisho wa mwaka wa fedha, wanatarajia kuvuka lengo hilo la kitaifa.




Katapila likipanua bonde la mto Ng'ombe lililopo eneo la kati ya kwa Mtogole na Ali Maua, wilayani Kinondoni, jijini Dar es Salaam, ili kuondoa mafuriko kwenye eneo hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Serikali yaondoa kodi kwa vifaa tiba corona

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

SERIKALI imeondoa kodi kwenye vifaa tiba vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi, ili kurahisisha upatikanaji wake katika kukabiliana na maambukizo ya virusi vya corona.

Pia, imeahirisha matumizi ya baadhi ya fedha zilizokuwa zimeshapangwa ikiwamo kusitisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo haijaanza kabisa na fedha hizo kuelekezwa kupambana na corona.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliyasema hayo bungeni juzi jijini Dodoma.

Alisema Aprili 16, mwaka huu, Waziri wa Afya alipeleka orodha ya vifaa 15 vya nyongeza vinavyostahili kusamehewa kodi kwa ajili ya kupambana na corona.

"Tulishatoa ridhaa na vifaa vyote hivi vitaingia nchini bila kulipiwa ushuru wa forodha, Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), lakini tumeweka masharti kidogo ili msamaha huo usitumike vibaya,"alisema.

Kwa mujibu wa waziri huyo, wamechambua mafungu mbalimbali ambayo matumizi yake yanaweza kuahirishwa ili kuelekeza fedha zake kwenye matumizi ya dharura na kuongeza kasi ya kulipa malimbikizo ya makandarasi, watoa huduma na watumishi ili kuhakikisha fedha zinawafikia.

Alisema kipaumbele ni kukinga watoa huduma za afya na wananchi na kwamba kwa kipindi cha Machi hadi Septemba mwaka huu, zinahitajika Sh. bilioni 382.5 kwa ajili ya kukabiliana na corona.

"Mpaka sasa, tumekwishatoa Sh. bilioni 15.49 kwa Bara na Sh. milioni 500 Zanzibar. Tunagharamia upatikanaji wa mahitaji ya msingi ambayo ni pamoja na vifaa vya kujikinga na kuwakinga watoa huduma, dawa, vifaa tiba, vitendanishi na kuongeza mashine za kupumulia, magari ya kubebea wagonjwa na kuimarisha kambi zilizopo.

"Tumeendelea kuhimiza sekta binafsi kuchangia mfuko wa maafa na hadi sasa zimepokewa Sh. bilioni 1.945 zilizoelekezwa kwenye vifaa vya kujikinga na inapunguza mzigo kwa serikali. Tunaomba fedha kutoka Shirika la Fedha Ulimwenguni zenye riba sifuri na masharti nafuu na tunatarajia kupata majibu," alisema.

Alisema kuwa juzi alipokea barua kutoka Benki ya Dunia (WB) ambao wamesema huenda wakasimamisha madeni kuanzia jana (Mei Mosi) hadi Desemba 31 mwaka

INAENDELEA UK.19

HABARI KITAIFA

# Mtoto afa kwa kung'atwa na fisi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SUNGWA Kulwa (3), mkazi wa Kijiji cha Dodoma, Kata ya Masanga, wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, amefariki dunia baada ya kushambuliwa na fisi.

Tukio hilo lilitokea Aprili 30 mwaka huu majira ya saa moja jioni, wakati mtoto huyo akiwa anacheza na wenzake umbali wa takribani mita 10 kutoka nyumbani kwao.

Akitoa taarifa jana kwa vyombo vya habari, Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema kuwa wakati watoto hao wakicheza, ghafla alitokea fisi kwenye kichaka kilichoko karibu na nyumba hiyo na kuanza kumshambulia mtoto huyo maeneo ya kichwani kisha kumburuza umbali wa takribani mita 100 na kusababisha kifo chake.

Kamanda Magiligimba alisema fisi huyo baada ya kusikia kelele za wananchi waliokuwa wakimfukuza, aliuachia mwili wa mtoto huyo na kukimbia.

"Mtoto Sungwa Kulwa mwenye umri wa miaka mitatu ameuawa na fisi wakati akicheza na wenzake nje ya nyumba yao umbali wa mita 10, fisi alitokea ghafla, akitoka vichakani na kushambulia sehemu za kichwani na kisha kumburuza umbali wa mita 100 na hatimaye kufariki dunia," alisimulia.

"Natoa wito kwa wazazi na walezi mkoani Shinyanga, kuhakikisha kwamba watoto wao kipindi wanacheza wawe katika mazingira salama muda wote na wasiachwe peke yao. Wananchi wachukue tahadhari hasa katika kipindi hiki, fisi wamekuwa wakionekana maeneo mbalimbali ya mkoa wetu," alionya.

Kiongozi huyo wa polisi alisema elimu ya wananchi namna ya kujikinga pamoja na utoaji wa taarifa mapema za wanyama wakali imeshatolewa na maofisa wanyamapori wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu.

Aliwakumbusha wananchi kuhakikisha wanatoa taarifa kwa mamlaka husika wanapoona wanyama wakali wakizurura ovyo mitaani.



Wasamaria wema wakimsaidia mwendesha pikipiki kuiinua kwenye daraja linalounganisha Kwa Mtogole na Kwa Alli Maua, baada ya kushindwa kupanda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Kalemani aamuru wadaiwa sugu kukatiwa umeme

**Na Zuena Msuya,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameliagiza Shirika la Umeme nchini (Tanesco), kuwakatia umeme wadaiwa sugu ili kukusanya mapato zaidi na kulipa madeni ya Shirika hilo.

Alisema hayo juzi jijini hapa, alipokutana na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Tanesco kuzungumzia tathmini ya miaka mitano ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, baada ya kufanya ziara ya kukagua ujenzi wa upanuzi wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Zuzu.

Dk. Kalemani aliiagiza Tanesco kuwakatia umeme wadaiwa sugu na kuwa kwa kufanya hivyo kutamaliza tatizo la wadaiwa hao.

"Tanesco inadaiwa madeni makubwa, pia ina wateja wengi sana ambao ni wadaiwa sugu wanaodaiwa fedha nyingi sana na hawalipi, zimo yaasisi, mashirika ya umma na binafsi, pamoja na watumiaji wa kawaida, ninawaagiza nendeni mkawakatie umeme! Narudia tena mkakate umeme! Mkishaukata, wahusika watalipa na wataonyesha ushirikiano mkubwa, tofauti na kumdai kawaida tu," alisema Dk. Kalemani.

Kuhusu wizi na uhujumu wa miundombinu ya umeme, Dk. Kalemani, aliitaka Tanesco, Bodi yake na watendaji wa Wizara ya Nishati, kushirikiana kutafuta njia sahihi na ya kisasa zaidi ya kubaini wizi wa umeme, unaofanywa na watu wasio waaminifu na kusababisha hasara kwa Shirika kupoteza mapato ya taifa.

"Wizi wa umeme upo na haukubaliki, tuweke mfumo sahihi wa kisasa kubaini wahusika, tuache hii tabia ya kukimbizana kimbizana na wezi, pia sisi watumishi tuwe wazalendo na wasimamizi wazuri wa miundombinu yetu, vilevile tuwe na walinzi wenye weledi katika miradi yetu bila kujali ni ya serikali au mtu binafsi, jukumu la ulinzi ni letu sote faida ya taifa kwa jumla,"alisisitiza Dk. Kalemani.

Aliwataka kuendelea kufanya tathmini na uwiano wa gharama za kutengeneza nguzo za zege na zinazotumika sasa ili kuangalia uwezekano wa kuzitumia katika maeneo yote nchini na kwa gharama nafuu na kuondoa tatizo la kuoza ama kuungua kwa nguzo hizo.

Vilevile alitaka kuongezeka kwa idadi ya wateja wa umeme katika kila sekta, kuharakisha uunganishaji wa umeme kwa mteja pale anapomaliza kulipia gharama husika, pamoja na kutatua changamoto za wateja kwa wakati sahihi ili kuvutia wateja wengi zaidi na kuondoa malalamiko.

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, aliitaka Shirika hilo kuangalia uwezekano wa kutoa zawadi kubwa kwa wasamaria wema wanaotoa taarifa za siri kuhusu wanaohujumu na kuiba umeme, tofauti na inayotolewa sasa ambayo pia huchukua muda mrefu kuikabidhi kwa muhusika.

Mgalu alikitaka kitengo husika kutunza siri za watoa taarifa, pia kifanye uchunguzi wa kina na kutoa adhabu kwa mtumishi yeyote atakayetiliwa shaka au kuhusika na wizi pamoja na kuhujumu miundombinu ya umeme kama inavyofanywa kwa wahusika wengine wanaobainika.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mhandisi Zena Said, alisema ili kukabiliana na changamoto ya wizi na uhujumu wa miundombinu ya umeme, watashirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kuimarisha ulinzi kuanzia ngazi za kaya.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Tanesco, Dk. Alexander Kyaruzi, aliishuruku Wizara ya Nishati kwa kuwapa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yao na kuyafanyia kazi yale waliokuwa wakiishauri wizara hiyo, katika kipindi chote cha miaka mitano.

# Madiwani wamkataa Meneja Tarura

**Na Manuel Kaminyoge, SONGWE**

MADIWANI katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi wamemkataa Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura),Wilaya ya Mbozi, Mhandisi Naftari Chaula, kwa madai ya kushindwa kutekeleza maagizo yanayotolewa na madiwani hao ikiwamo kushindwa kuwasilisha mpango wa bajeti.

Walidai kuwa tabia ya meneja huyo kushindwa kutekeleza maagizo yao katika vikao halali vya kisheria inaweza kuwachonganisha na wapiga kura wao ambao baadhi yao wameshindwa kufanya shughuli zao baada ya madaraja kuvunjika na Tarura kushindwa kwenda kusaidia kurejesha huduma.

Uamuzi huo ulitolewa jana katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wakati wakithibitisha ajenda zilizopangwa kujadiliwa na Diwani wa Kata ya Nyimbili, Tinson Nzunda (CCM), kusimama na kutoa hoja ya kumkataa Meneja Chaula na kuiomba mamlaka zilizomteua zimpangie sehemu nyingine ya kufanya kazi.

Hoja ya diwani huyo iliungwa mkono na baadhi ya madiwani, hali iliyomlazimu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Erick Ambakisye, kuwataka madiwani hao kufanya hitimisho la hoja hiyo kwa kuweka maazimio.

Ushauri wa Mwenyekiti ulikubaliwa na kilifika kipengele cha kuwahoji na diwani 22 waliunga mkono hoja ya kumkataa meneja huyo na wengine wanane walipinga kuondolewa kwake.

Awali, Diwani wa Kata ya Ipunga, Button Sinienga, akichangia ajenda kabla ya kuibua hoja ya kukataliwa kwa meneja huyo, alisema hana ushirikiano na ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri na mara kadhaa amekaidi kuwasilisha mpango wa bajeti ya taasisi hiyo kama taratibu na miongozo inavyotaka.

Naye Diwani wa Hezya, Willy Mukondya, alimlalamikia meneja huyo akidai kumdanganya kumpa fedha za ujenzi wa barabara ya Hezya hadi Namwangwa yenye urefu wa kilometa 11 ambayo ni kero ya muda mrefu kwa wananchi wa kata yake.

Akizungumza nje ya ukumbi, Meneja wa Tarura aliyekataliwa, Chaula, alionyesha kushangazwa na taarifa za kukaidi kupeleka mpango wa bajeti kwenye vikao vya halmashauri kwa kuwa alitekeleza agizo hilo kwa kupeleka taarifa hiyo katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya, John Palingo na nakala kupeleka kwa Mkurugenzi, akiamini kuwa ingewafikia madiwani hao.

"Barua ya kuitwa kwenye kikao na kuwasilisha mpango wa bajeti ya ofisi yangu nilipata jana (juzi) na haraka mimi na timu yangu tuliandaa taarifa ya bajeti na kuipeleka kwa (DC) Mkuu wa Wilaya na nakala kuipeleka kwa Mkurugenzi, sasa hoja ya mimi kukaidi nashangaa inatoka wapi," alisema.

Katika hatua nyingine Baraza hilo lilitoa siku 14 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Hanji Godigodi, kutekeleza maagizo manne kinyume na hapo hatua zaidi zitachukuliwa dhidi yake.

Mkurugenzi Godigodi, hata hivyo, aliwaomba radhi madiwani hao na kuahidi kutekeleza maagizo yaliyotolewa ikiwa ni pamoja na umaliziaji wa kituo cha afya Ndolezi kilichojengwa kwa nguvu za wananchi na serikali kuu kutoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya umaliziaji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji wavivu Bara kuumbuliwa na Corona

**HUKU** mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na Ligi Kuu ya Wanawake nchini zikiwa zimesimama kutokana na kuenea kwa ugonjwa wa Corona, wachezaji wa ligi hizo wote wanatakiwa kuendelea kufanya mazoezi binafsi ili kulinda viwango vyao.

Ugonjwa huo umegusa sekta mbalimbali na kufanya mtikisiko ambao umeshaleta na unatarajiwa kuleta maumivu ndani ya mioyo ya watu.

Kwa sababu hali si shwari na mambo mbalimbali hapa duniani yakiwa yamesimama kutokana na kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona (COVID 19), wanamichezo wenyewe wanalazimika kuendelea na mazoezi.

Wanamichezo hao wanatakiwa kufanya mazoezi kwa kufuata programu maalumu kutoka kwa makocha wao, kwa sababu ya kujiweka tayari na mshikemshike wa mechi za ligi hizo zitakaporejea.

Licha ya wanamichezo hao kukumbwa na changamoto katika kufanya mazoezi, bado jambo hilo haliwafanyi kuacha kujifua.

Wanamichezo wanatakiwa kujifua na kujiimarisha huku wakichukua tahadhari, kwa sababu ligi zitakaporejea wanatakiwa kuzisaidia timu zao kumaliza vema msimu wa mwaka 2019/20.

Ingawa kuna baadhi ya nchi kama Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi na majirani zetu Kenya kuwa hazitarejea tena, lakini hapa nchini wachezaji wanatakiwa kuendelea na mazoezi kwa matumaini msimu utaendelea na hatimaye kupata bingwa na kufahamu timu zitakazoshuka daraja.

Nipashe inawakumbusha wachezaji wavivu kuacha kutegea kwa sababu mara ligi zitakaporejea, wataumbuka kwa kucheza katika viwango vya chini.

Mchezaji ambaye atakuwa 'anakacha' mazoezi, hatakuwa anaikomoa klabu yake, atakuwa anajiweka katika mazingira magumu ya kuendelea kuaminiwa na klabu aliyopo.

Mbali na kumalizia msimu, kipindi kilichosalia bado ni muhimu kwa wachezaji wetu kwa sababu dirisha la usajili litakuwa limekaribia na hivyo wachezaji watakaoonyesha ubora, watajitengenezea nafasi ya kupata mikataba mipya na yenye mslahi bora.

Huu si wakati wa mchezaji 'kuponda raha' na badala yake wanatakiwa kufuata kikamilifu ratiba za mazoezi walizokabadhiwa ili pale watakaporejea uwanjani wawe kwenye viwango vya juu na si kuanza upya.

Licha ya mchezaji kubainika alikuwa hafanyi mazoezi, lakini itawaepusha na majeraha yasiyotarajiwa ambayo yanaweza kuwaathiri nyota hao kutokana na 'ujinga' wa kujitakia.

Kila mchezaji ni lazima awe balozi wa kulinda kiwango chake kwa sababu katika soka, mechi za hatua ya lala salama huwa na changamoto zaidi ukilinganisha na michezo ya kufungua msimu.

Hakuna kisichowezekana, huu ni wakati wa kila mwanamichezo, hususani wa soka kufuata kwa umakini program walizopewa bila kukosea kwa sababu soka ni kazi inayoendesha maisha yao kwa sasa.

Ni wakati wa wachezaji kujipanga wenyewe wakiwa nyumbani na uzuri ni kwamba ratiba inakuwa mikononi mwao wenyewe wanajua namna ya kuipanga kiusawa bila kupangiwa na endapo watashindwa kuwa waaminifu katika kipindi hiki cha corona, basi timu zao zitarajie kuvuna matokeo mabaya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kinga na kinga ndipo...

Na Barnabas Maro

**HUSEMWA** "Kinga na kinga ndipo moto huwakapo." Maana yake moto huwaka baada ya kijinga kimoja kuunganishwa na kijinga kingine cha moto. Hii ni methali ya kutufunza faida zinazotokana na kushirikiana.

Kadhalika "Kinolewacho hupata (hukata)." Maana yake kitu kinachonolewa kama vile kisu au upanga/panga, huishia kupata makali na kuweza kukata. Methali hii yatufunza kuwa tuanzapo kufanya jambo kwa uangalifu na bidii mara kadha, hatimaye tunaishia kufanikiwa au kulimudu vizuri.

Msimu wa usajili wa wachezaji wa kandanda, hasa kwa timu za Ligi Kuu ya Tanzania Bara, tayari umeanza kama kawaida kwa Simba na Yanga kuviziana na kuvutana katika usajili. Mara nyingi timu hizo kongwe hushindana kwa fedha ili kuwapata wachezaji wanaokusudia kuwasajili.

Katika mvutano huo, kuna wachezaji wa aina mbili au tatu. Wapo wanao jirahisisha kwa timu wazipendazo. Wachezaji wa fungu hili ni wale wawekao mapenzi yao kwa timu wazipendazo kuliko fedha. Hawa, abadan hawajali hata kama huko waendako kuna wachezaji hodari na madhubuti (imara, -enye kuhimili mikiki) kuliko wao!

Shabashi! (tamko la kupongeza linalodhihirisha hisia ya furaha). Hata wahenga walisema "Kipendacho moyo ni dawa" na "Kipenda roho hula nyama mbichi" wakimaanisha kuwa kitu anachokipenda mtu au inachokipenda roho ya mtu huwa ni kama dawa yake. Methali hii hutumiwa kumpigia mfano mtu anayeelekea kukipenda kitu fulani sana ingawa wengine wanakiona kuwa cha kawaida au kibaya.

Wachezaji wa aina ya pili ni wale wanaojiunga na vilabu hivyo ili kupata hela nyingi kuliko timu wanazozitumikia. Hawa hata kama wakiwekwa ubaoni bila kucheza kwa muda mrefu, hawajali alimradi (bora tu) wanapata hela zaidi ya kule wanakotoka. Katika kundi hili, pia wamo wanaodanganyika kwa magari na simu za bei kubwa!

Malengo yao ni kuwa na magari ya fahari (jambo au kitu bora cha kujivunia kwa watu; utukufu unaotokana na hadhi ya mtu katika jamii) ya kuzurura mitaani ilhali bado wapo kwa wazazi wao au ni wapangaji! Wanapohojiwa na vyombo vya habari kuhusu vitu wanavyopenda kuvimiliki maishani, haraka hutaja magari, simu na saa, vyote vya bei kubwa!

Wachezaji wa aina hiyo hawajui kuna leo na kesho! Sawa, chukua gari. Uwezo wako wa kucheza kandanda utapungua, timu inakuacha kwenye usajili ilhali bado upo kwenye nyumba ya kupanga, utakuwa mgeni wa nani? Utatembea mitaani na gari lenye mafuta ya kuombaomba kwa marafiki, mipira mibovu na kushindwa gharama za matengenezo. Mwishowe utashindwa hata kuhuisha leseni ya gari! Kama vyote hivyo vyakushinda, utalipaje kodi ya chumba unachopanga?

Kwa wazazi wako kuna wapangaji ambao ndio tegemeo lao. Je, wafukuzwe ili utunzwe na wazazi wako badala ya kuwatunza wewe? Ulipokuwa ukitamba mitaani na gari lako huku ukiwabadili 'wale jamaa' kama nguo, hukuwajali wazazi wako!

Lahaula! (neno linalodhihirisha mshangao au sikitiko; tamko linalotumiwa na mtu anapotanabahi (kitendo cha mtu anapokumbuka jambo; zinduka baada ya kusahau au kushtukia jambo).

Mungu ametaka kwamba, "baada yake tuwaheshimu wazazi wetu ambao tunawiwa uhai wetu na waliotupatia ujuzi wa Mungu. Hatuna budi kuwahehimu na kuwastahi wale wote ambao Mungu amewapa mamlaka yake kwa faida yetu." (Katekisimu ya Kanisa Katoliki Uk. wa 488-489).

Aina ya tatu ni wachezaji wanaotafuta uwezekano wa kusajiliwa na timu za nnje ya Tanzania, hasa Ulaya na Marekani. Kwa hiyo huzifanya Simba na Yanga kama ngazi za kupandia au kioo kinachowaonesha kwa timu zinazohitaji wachezaji kutoka Afrika.

Neno *shughuli maana yake ni jambo ambalo utendaji wake unamtaka mtu atumie nguvu na akili; kazi. Hakika wacheza kandanda hutumia nguvu na akili kwani kwao ndio kazi. 'Shughulikia' ni kitendo cha mtu kuelekeza nadhari (ufahamu wa jambo; mazingatio) zake kwenye jambo. Ndivyo wafanyavyo wacheza kandanda wanapokuwa uwanjani kutafuta ushindi dhidi ya timu wanazopambana nazo.

Wachezaji wa sasa hawapaswi kujilinganisha na wale wa zamani kwani kuna mabadiliko makubwa ya maisha. Zamani walicheza ili kuwafurahisha watazamaji na kuweka miili yao katika hali nzuri. Kuna waliocheza kwenye timu za Simba na Yanga kwa kupelekwa na wazazi wao na waliojipeleka kwa mapenzi yao wenyewe.

Sasa kandanda ni kazi inayolipa, tena kwa hela nyingi. Wachezaji wa sasa wanapaswa kujali kazi yao ya uchezaji ili kuwa na maisha mazuri kama wenzao huko Ulaya na Marekani.

Waige mfano wa Mbwana Samatta ambaye amewajengea wazazi wake nyumba nzuri na kujijengea jumba lake ya kifahari. Kama hiyo haitoshi, anamshukuru Maulana kwa kumwezesha yote hayo na sasa anaombewa mema na waumini wanaosali kwenye Msikiti aliojenga kule Kigamboni.

marobarnabas@yahoo.com
0784 334 096

# Wakabidhi kwa RC vifaa kukabili corona

**Na Francis Godwin,** IRINGA

KAMPUNI ya kizalendo ya Qwihaya General Enterprises ya mkoani Iringa, imekabidhi msaada wa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 12 kwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, ili kusaidia jitihada za serikali kukabili maambukizo ya virusi vya corona.

Chini ya Mkurugenzi wake, Leonard Mahenda, kampuni hiyo ilikabidhi msaada huo jana kwa Mkuu wa Mkoa, Ally Hapi, ikiwa ni sehemu ya kampuni kuunga mkono jitihada za serikali katika mapambano dhidi ya corona.

Mhenda alisema wameguswa na kutoa misaada hiyo wakiamini kwamba njia sahihi na salama ya kujikinga na baa hilo ni kwa kuwa na vifaa vya kujikinga na kuvitumia ipasavyo.

Vifaa vilivyotolewa ni pamoja na mavazi 20, vitakasa mikono lita 75, sabuni za maji lita 100, vipima joto sita, barakoa na matenki makubwa ya kunawia maji 62, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 12.

Kwa upande wake Hapi, akipokea msaada huo na wa wadau wengine, alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kufuatilia uvaaji wa barakoa na unawaji wa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka katika vyombo vya usafiri na sehemu zote za biashara.

Msaada huo uliotolewa na taasisi nyingine tano unahusisha mavazi maalum ya watoa huduma (PPE), vipima joto, vitakasa mikono, sabuni, barakoa, matenki ya maji na barakoa maalum zinazovaliwa na matabibu wakati wa upasuaji.

Alisema tayari ugonjwa huo umeingia mkoani Iringa na akawataka wananchi kuzingatia maelekezo ya wataalamu ili kujikinga na maambukizo.

Taarifa iliyotolewa na kiongozi huyo, ilieleza kuwa, mtu mmoja aliyetokea Dar es Salaam, alifariki dunia April 19 mwaka huu kutokana na corona.

Akiwashukuru wadau wote wanaounga mkono mapambano ya kutokomeza ugonjwa huo kwa kutoa misaada ya vifaa na vifaa tiba, Hapi alizikumbusha kamati mbalimbali ziendelee kufuatilia utekelezaji wa mikakati ya kudhibiti ugonjwa huo.

# Hakimu mbaroni tuhuma za rushwa

**Na Ambrose Wantaigwa, TARIME**

HAKIMU Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Tarime, Bhoke Chacha, anashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(Takukuru) mkoa wa Mara, kutokana na tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni mbili

Mkuu wa Takukuru mkoani Mara, Alex Kuhanda, alisema mjini Musoma jana kwamba, mtuhumiwa huyo anadaiwa kupokea kiasi hicho cha fedha kama ushawishi wa kutoa upendeleo katika kesi iliyokuwa mbele yake ya mlalamikaji ambaye hakutajwa jina kutokana na sababu za kiusalama na upelelezi.

Alisema ofisi yake ilipokea taarifa kutoka kwa mlalamikaji huyo ambaye pia ni mfanyabiashara kwamba hakimu huyo alimwomba kiasi hicho cha fedha ili kumpa upendeleo katika kesi ya msingi ya madai ya mafao.

Mtendaji huyo wa Takukuru alisema mlalamikaji alitoa taarifa kwenye taasisi hiyo ambayo iliweka mtego na kufanikiwa kumnasa na fedha hizo.

Inadaiwa mtuhumiwa huyo alidiriki kutoa uamuzi katika kesi hiyo akiwa nyumbani kwake wakati alikuwa katika likizo ya uzazi, kinyume cha taratibu za kisheria zinazoelekeza mashauri kusikilizwa na kutolewa uamuzi mbele ya mahakama.

"Mtuhumiwa huyo wakati akiomba kupatiwa fedha hizo alikuwa katika likizo ya uzazi nyumbani kwake, anadaiwa kumshawishi mlalamikaji kwamba angempa upendeleo wa kumsaidia kupata malipo yake ya mafao katika kesi ya msingi aliyokuwa anaisikiliza," alisema.

Kuhanda pia alisema taasisi hiyo imefanikiwa kuokoa Sh. milioni 159 mkoani hapa kutokana na vitendo vya wakopeshaji binafsi wanaoweka riba kubwa kwa wakopaji wao ambao mara nyingi ni watumishi wa umma.

Alisema wameanzisha uchunguzi kuhusu taasisi binafsi zinazokopesha watumishi na raia wengine zilizozagaa katika maeneo mbalimbali mkoani hapa na wamebaini mara nyingi hazijasajiliwa na zinafanya kazi yake kinyume cha taratibu zinazosimamia biashara ya kifedha nchini.

"Mara nyingi wakopeshaji hawa wamekuwa wanaweka riba kubwa kwa wakopaji wao ambao wengi ni watumishi wa umma na hivyo kusababisha usumbufu wakati wa kudai mafao yao kwa kuwa wanalazimika kusalimisha hati za msingi ikiwamo kadi za benki," alisema.



Mbeba mizigo katika soko maarufu kama 'mahakama ya ndizi' Mabibo jijini Dar es Salaam, akiwa amebeba mzigo wa mteja wake akiwa pekupeku kwenye matope yaliyojaa kwenye soko hilo kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha nchini. **PICHA:JOSEPH MWENDAPOLE**

# Uchezeaji vipimo waponza wafanyabiashara

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WAKALA wa Vipimo mkoani Shinyanga, umekusanya jumla ya Sh. milioni 19 kutoka kwa wafanyabiashara mkoani hapa waliokamatwa kwa kuchakachua vipimo vya mizani, vifungashio na kuwaibia wananchi.

Hayo yalibainishwa juzi na Kaimu Meneja Wakala wa Vipimo mkoani Shinyanga, Hilolimus Mahundi, alipozungumza na Nipashe kuhusu mikakati yao ya kuwabana wafanyabiashara wenye tabia ya kuchezea vipimo vya mizani pamoja na vifungashio na kuwaibia wananchi.

Alisema katika kipindi cha robo tatu ya mwaka kilichoanzia Juni 2019 hadi Machi mwaka huu, walifanya ukaguzi wa kushitukiza kwa wafanyabiashara 80 mkoani hapa na kati yao, 19 waliwakamata kwa kukiuka Sheria ya Vipimo na kuwapiga faini ya kulipa Sh. milioni moja kila mmoja.

"Kabla ya kukamata wafanyabiashara, huwa kwanza tunatoa taarifa na kufanya ukaguzi wa kawaida wa vipimo, na baada ya hapo tunafanya ukaguzi wa kushitukiza ili kujiridhisha kama hawajachezea tena vipimo hivyo, na ambao tunawakamata ndiyo tunawapiga faini, wakigoma tunawapeleka mahakamani.

"Wafanyabiashara ambao tuliwakamata kwa kukiuka Sheria ya Vipimo ni wanunuzi wa zao la pamba, tumbaku, vifungashio vya bidhaa mbalimbali ikiwamo sukari, pamoja na vituo vya kuuza mafuta, na zoezi hili tumepanga kulifanya tena wiki ijayo," alisema.

Naye Ofisa Biashara Mkoa wa Shinyanga, Pastor Mfoy, alisema kumekuwapo na tatizo kubwa kwa wafanyabiashara wa vifungashio hasa katika Wilaya ya Kahama, kuchakachua vipimo vya bidhaa ikiwamo sukari ili kuwaibia wateja wao.

Alisema kuna haja uuzaji wa bidhaa hizo ufanyiwe ukaguzi hasa kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona na mfungo wa Ramadhani.

HABARI KITAIFA



Ofisa Muuguzi wa chumba cha upasuaji kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Aimana John, akiwaelekeza wauguzi wenzake namna sahihi ya kunawa mikono kwa majisafi yanayotiririka na sabuni, wakati wa mafunzo ya jinsi ya kupambana na ugonjwa wa Corona (COVID-19) yanayotolewa kwa wafanyakazi wa Taasisi hiyo. **PICHA: ANNA NKINDA**

# ACT waruhusu wagombea 2020 kuanza kujitangaza

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimefungua milango kwa wagombea wa nafasi za urais, ubunge na udiwani, kuanza kujitokeza na kujitangaza katika mitandao ya kijamii na vyombo vya habari na kujiorodhesha katika daftari la watia nia.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa, ameagiza makatibu wa kata na majimbo wa chama kuandaa madaftari ya kuorodhesha watia nia katika maeneo yao ili kupata idadi ya watia nia.

"Mwanachama yeyote anayetaka kugombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, milango iko wazi kutangaza nia, Zanzibar milango iko wazi vilevile, wanaotaka kugombea ubunge na udiwani, milango iko wazi kutangaza nia," alisema.

Ado aliwataka watia nia hao kuzingatia maadili, utu na utamaduni wa chama hicho wanapotangaza nia na kuomba msaada wa kuunganishwa na vyombo vya habari ili kujitangaza inapobidi katika Idara ya Uenezi ya chama hicho.

Tayari chama kikuu cha upinzani nchini, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimefunga dirisha la watia nia kujitokeza kuanzia Machi 30 mwaka huu huku ikielezwa kuwa watia nia zaidi ya watatu katika kila jimbo wamejitokeza ikiwamo 72 waliojitokeza katika majimbo yaliyopo katika Jiji la Dar es Salaam pekee.

Kati ya wanachama wa Chadema waliojitokeza kuwania nafasi hizo, wapo waliotia nia kuwania ubunge kwenye majimbo ambayo tayari yana wabunge wa upinzani kupitia chama hicho.

Hata hivyo, kwa nafasi ya urais, chama hicho kupitia Mkurugenzi wake wa Mambo ya Nje, Itikadi na Uenezi, John Mrema, kilisema hakijafungua milango, lakini kanuni za chama hicho zinaruhusu yeyote mwenye nia ya kugombea kiti hicho kumwandikia barua Katibu Mkuu wa chama hicho na kueleza nia yake.

***Imeandikwa na Enock Charles na Elizabeth Zaya**

# 'Kampuni za simu zishushe gharama'

**Na Elizabeth Zaya**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umeoziomba kampuni za simu, watoa huduma za intaneti na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), kupunguza gharama za huduma na bidhaa zao kwa wateja katika kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona.

Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao huo, Onesmo Olengurumwa, alisema jana kuwa, tangu serikali itangaze kuwapo kwa ugonjwa huo nchini, hali ya uchumi imeyumba kutokana na baadhi ya biashara na ofisi kufungwa na baadhi ya wafanyakazi kufanyia kazi zao nyumbani.

"Kwa hali ya sasa, ni dhahiri kwamba wanafunzi, walimu, wafanyabiashara, watetezi wa haki za binadamu, wafanyakazi wa Azaki zilizofunga ofisi zao pamoja na familia nyingi zimelazimika kukaa na kufanyia shughuli zao majumbani.

"Bila shaka, hali hii imeziongezea faida maradufu kampuni na mitandao ya simu, kampuni za huduma ya intaneti na Tehama kwa kuwa vifaa vya mawasiliano kama vile simu na kompyuta ndiyo njia mbadala za mawasiliano kwenye jamii katika kipindi hiki cha janga la corona," alisema.

Olengurumwa alisema ni vyema kampuni hizo zikapunguza gharama za huduma na bidhaa zao na kuwa wabunifu kwa kutoa bando zenye bei nafuu ili kuwapa unafuu wa huduma ya mawasiliano Watanzania katika kipindi hiki ambacho wanafanyia kazi zao majumbani na wanafunzi wanatumia intaneti hiyo kwa ajili ya kujifunza.

Aliiomba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kutoa agizo kwa kampuni hizo kupunguza gharama za huduma zao ikiwamo kuwaelekeza kutoa baadhi ya huduma zao bure katika kipindi hiki ikiwamo Wi-Fi za bure hususani katika maeneo ya vituo vya mabasi.

"Huu ni muda mwafaka kwa TCRA pia kupunguza au kuondoa kabisa gharama za usajili wa mitandao kama vile YouTube na blogu ili walimu watumie kuwafundishia wanafunzi," alisema/

Olengurumwa pia aliishauri Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mamlaka ya Mapato (TRA), kupunguza kodi ya huduma za intaneti kwa watoa huduma, ili Watanzania wanufaike na matumizi ya intaneti katika kipindi hiki.

Vilevile, aliwashauri wafanyabiashara kutumia zaidi mitandao kufanya mauzo ya bidhaa na huduma zao ili kupunguza misongamano isiyokuwa ya lazima madukani.

# Wasimamizi watahadharishwa maambukizo corona

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

OFISA Mwandikishaji wa Jimbo la Iringa Mjini ambaye ni Mkurugenzi wa Manispaa, Hamid Njovu, amewataka wasimamizi wasaidizi ngazi ya kata na waandishi wasaidizi kutokuwa chanzo cha maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya wasaidizi ngazi ya kata na waandishi wasaidizi, mjini hapa.

Njovu alisema katika uboreshaji daftari la wapigakura awamu ya pili ya uandikishaji, suala la mapambano dhidi ya virusi vya corona limezingatiwa kwa dhati na kutoa wito wa kuhakikisha wanajua utaratibu unaotakiwa katika mchakato mzima wa uchaguzi.

Alisema, madhumuni ya mafunzo hayo ni kuhusu uandikishaji wa wapigakura katika daftari la kudumu na uboreshaji wa wapigakura awamu ya pili ambao utafanyika katika vituo 18 vilivyopo kwenye kata katika Manispaa ya Iringa.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ipo mkoani Iringa kwa ajili ya uandikishaji wapigakura katika daftari la kudumu na uboreshaji wa wapigakura awamu ya pili na kwa Manispaa ya Iringa utafanyika katika vituo 18 kuanzia Mei 2 hadi 4, mwaka huu.

"Ninaomba nitumie nafasi hii kuwakumbusha tena juu ya unyeti wa jukumu la kuwaelekeza wapigakura kuwa ni muhimu sana kuwaelewesha wananchi kutumia haki yao ya kupiga kura kwa kuzingatia maelekezo ya Tume ya Uchaguzi kikamilifu," alisema Njovu.

Pia, aliwakumbusha kuwa uchaguzi ukivurugika madhara ni yake ni makubwa kwa amani ya nchi na ni madhara ya muda mrefu na pia ni hasara kwa taifa kwa kuwa serikali inatumia fedha nyingi katika uchaguzi.





# Wataka serikali ilipe mabilioni ya walimu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Walimu (CWT), kimeitaka serikali kulipa madeni mbalimbali ya walimu yanayofikia Sh. bilioni 38.34, ili kuchochea ari na maendeleo ya ufanyaji kazi wa kada hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, alisema hadi kufikia Desemba 2019, serikali ilikuwa imefanikiwa kulipa madeni ya Sh. bilion 8.7, hivyo kuiomba kulipa kiasi kilichobaki.

"Eneo la madeni yatokanayo na uhamisho na ufungaji mizigo kiasi cha Sh. bilioni 2.9 zimeshalipwa, madeni ya kwenda masomoni ni Sh. bilioni 21.5," alisema.

Kiongozi huyo wa CWT alisema walimu wana kazi kubwa, hivyo ni vyema serikali ikawaangalia kwa 'jicho la tatu' hususani katika siku ya wafanyakazi, jana.

"Tunashukuru kiasi cha fedha ambacho kimelipwa. Tunaiomba serikali imalizie madeni ambayo yamebaki, ili walimu waendelee kuwa na moyo wa kufanya kazi kama ilivyo kawaida yao," alisema.

Akizungumzia Siku ya Wafanyakazi, Katibu Mkuu huyo alisema ni muhimu kwao na wafanyakazi wengine, hivyo kila sekta ijikite katika kufanya mabadiliko katika utendaji wao wa kazi.

**Tunashukuru kiasi cha fedha ambacho kimelipwa. Tunaiomba serikali imalizie madeni ambayo yamebaki, ili walimu waendelee kuwa na moyo wa kufanya kazi kama ilivyo kawaida yao**

# TPSF: Urejeshaji mikopo usimamishwe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) Jiji la Dodoma, Ringo Iringo, ameishauri serikali kuzungumza na taasisi za kifedha ambazo zimetoa mikopo kwa wafanyabiashara, kusimamisha ulipaji wa marejesho au kupunguza riba kutokana na biashara kuathiriwa na ugonjwa wa corona.

Alitoa rai hiyo jana jijini, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu athari za virusi vya corona katika sekta ya biashara nchini.

Alisema mlipuko wa ugonjwa wa corona umeathiri wafanyabiashara wote, akibainisha kuwa hali hiyo inatishia hatma yao kutokana na wengi wao kuendesha shughuli zao kwa mikopo kutoka taasisi mbalimbali za fedha.

Iringo alisema ili kuwasaidia wafanyabiashara waliofunga biashara zao kutokana na kudorola kwa uchumi duniani kote, serikali haina budi kukutana na taasisi za kifedha nchini, ili kuona namna bora ya kuwasaidia.

"Biashara nyingi sana hivi sasa zimefungwa kama hapa Dodoma kuna viwanda vya kuzalisha mvinyo vimefungwa zaidi ya mwezi mmoja sasa, lakini hoteli ambazo zinategemea wageni kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi zimefungwa pia," alibainisha.

Alisema kama serikali itakutana na taasisi za kifedha na kujadiliana namna bora ya kuwasaidia wafanyabiashara, itawasaidia kuwapunguzia msongo wa mawazo walio nao kwa sasa kutokana na wengi wao kuendesha biashara zao kwa mikopo.

Vilevile, aliziomba mamlaka za mapato za mikoa nchini kupitia mameneja wa mikoa kukutana na viongozi wa jumuiya za wafanyabiashara kujadiliana namna ya kuikabili hali hiyo wakati huu wa mlipuko wa virusi hivyo.

Alisema mameneja wa mikoa wa Mamlaka ya Mapato (TRA), wanatakiwa kukutana na jumuiya hizo za wafanyabishara ili kujadiliana namna ya kusimamisha au kuongeza muda wa kulipa kodi pamoja na tozo mbalimbali wakati huu wa janga la corona.

"Hiki ni kipindi cha mpito, lazima mamlaka husika zikutane na wafanyabiashara ili kuona namna bora ya kupata suluhu ya dharura hii ambayo imetokana na janga la corona ambalo limesababisha uchumi wa dunia nzima kudorora," alishauri.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi (kushoto), akipokea misaada ya vifaa vya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa covid – 19, vilivyotolewa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu kazi, ajira na vijana, Athony Mavunde, kwa ajili ya kusambaza maeneo mbalimbali ya mikusanyiko ya watu jijini Dodoma jana.**PICHA PETER MKWAVILA**

# Wabuni kifaa kinachozuia kushika usoni

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

VIJANA wa Shirika la Ubunifu wa Teknolojia za Afya na Ulemavu nchini, wamebuni kifaa kinachozuia mtu kujishika usoni ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu (COVID-19).

Hayo yalibainishwa jana, na kiongozi wa shirika hilo, Hashimu Lihumbo, alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu teknolojia hiyo waliyoibuni.

Lihumbo alisema kundi lao linalojishughulisha na teknolojia za afya na ulemavu, wameona ni wakati sasa waje na teknolojia ya kutengeneza kifaa hicho kinachomzuia mtu kujigusa sehemu za uso wake kwa lengo la kuzuia maambukizo ya ugonjwa wa corona.

"Kifaa hiki kitamkumbusha mtu pale atakapotaka kunyanyua mkono wake juu moja kwa moja, kifaa hicho kitamzuia na mhusika kukumbuka kuwa asiguse uso, kwani anaweza kupeleka virusi vya corona sehemu hizo za macho pua na mdomo," alisema.

"Kundi letu tulibaini kuwa pamoja na elimu inayotolewa na wataalamu wa afya kuhusu watu kujikinga na maambukizo ya homa ya corona kwa kuzuiwa kujigusa usoni, bado wengi wanashindwa, tukaona tuje na teknolojia hii ya kumkumbusha mtu asijiguse usoni," alisema.

**Kundi letu tulibaini kuwa pamoja na elimu inayotolewa na wataalamu wa afya kuhusu watu kujikinga na maambukizo ya homa ya corona kwa kuzuiwa kujigusa usoni, bado wengi wanashindwa, tukaona tuje na teknolojia hii ya kumkumbusha mtu asijiguse usoni**

Aliongeza kuwa kifaa hicho kinafungwa kwenye kiwiko cha mikono kwa lengo la kuzuia mikono yake kujigusa usoni ili kuepuka kupeleka maambukizo ya ugonjwa huo.

"Teknolojia iliyotumika kutengeneza kifaa hiki haizuii mtu kufanya kazi zake za kawaida kama kuandika, kulima na kufanya kazi nyingine nyingi, lakini ukitaka kukunja mkono kupeleka usoni itakuzuia na kukumbuka kuhusu ugonjwa huu unaosumbua dunia,"alisema.

Kiongozi huyo alisema kuwa katika utafiti wao waliofanya kwa watu 76, watu 50 walisema wamefanikiwa kujizuia kugusa uso wao na kuifurahia teknolojia hiyo.

Alisema wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa fedha katika kutengeneza vifaa vingi kutokana na gharama kubwa, hivyo waliiomba serikali kuwasaidia kuzalisha vifaa vingi zaidi.

Alitaja gharama za kutengeneza kifaa kinachofungwa katika kiwiko cha mkono mmoja kuwa ni Sh. 2,000 hadi 3,000, lakini wakiwezeshwa gharama hizo zitapungua.

"Sisi hatuhitaji kunufaika wenyewe kama serikali itatusaidia kutengeneza, tutatoa ajira kwa vijana wengine kusambaza teknolojia hii ili kujikinga na huu ugonjwa," alisema.





# Wapigwa marufuku kuingia sokoni bila barakoa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Soko Kuu la Darajani eneo la Mji Mkongwe wa Zanzibar, limepiga marufuku wananchi na wafanyabiashara kuingia katika eneo hilo bila ya kuvaa barakoa ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya kupunguza maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Mkuu wa soko hilo, Shawal Abdul-Rahman, alisema Soko la Darajani ni miongoni mwa maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa wananchi kwa hivyo juhudi za tahadhari zinahitajika kuchukuliwa.

Alisema hata ratiba za uendeshaji wa soko hilo zimebadilika na sasa shughuli zitaanza asubuhi na kufungwa jioni saa 10.

Alisema wananchi wote watakaoingia katika eneo la soko hilo watalazimika kufuata masharti yaliyowekwa kwa ajili ya kujilinda na ugonjwa wa corona ikiwamo kunawa mikono na kutumia vitakasa mikono.

"Tumeweka utaratibu mpya wa shughuli za Soko Kuu la Darajani, sasa litafunguliwa mapema saa mbili na kufungwa saa kumi na watu watakaohitaji huduma watalazimika kufuata masharti ikiwamo kuvaa barakoa na kunawa mikono," alisema.

Alisema soko hilo linatembelewa na wananchi mbali mbali ikiwamo wageni kwa ajili ya kupata mahitaji muhimu ya kijamii ikiwamo chakula hivyo tahadhari za kuepukana na ugonjwa wa corona zinahitajika.

Alisema hakuna uhaba wa vyakula vya matunda vinavyotumika katika mwezi Mtukufu wa Ramadhan kama ndizi, mihogo na vyakula vya nafaka.

Alisema hata bei ya bidhaa hizo zimeshuka kufuatia upatikanaji wake kwa wingi kutoka vijijini na kisiwa cha Pemba.

"Tunapokea vyakula vingi aina ya ndizi na muhogo, bei yake imeshuka sana na hivyo kuwafanya wananchi wa kawaida kumudu gharama ya kununua vyakula hivyo," alisema.

Licha ya kutokuwapo kwa upungufu wa chakula cha futari, lakini kuna upungufu wa nazi.

Nazi moja inauzwa kati ya Sh. 1,000 hadi 1,500, bidhaa hiyo inatumika kwa wingi kipindi hiki cha Ramadhani.

# Wagonjwa corona watoa ushauri kwa serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAGONJWA wa corona wameshauri kuwa ni vyema kufanyiwa vipimo kwa mara nyingine kabla ya kuruhusiwa kurudi nyumbani kwao baada ya kutokuwa na dalili za ugonjwa huo.

Walisema kuwa hali hiyo itawafanya kutokuwa na wasiwasi kuliko kuruhusiwa kutoka hospitali bila ya kufanyiwa vipimo.

Wakizungumza na Nipashe wagonjwa hao ambao hawakutaka kutajwa majina yao, walisema hivi sasa wagonjwa waliopona na kutokuwa na dalili zozote za corona wanaruhusiwa kutoka hospitali bila kufanyiwa vipimo kwa mara ya pili.

"Ingawa tumeambiwa kuwa tumeshapona corona, lakini kwa kweli bado tunahofu tunaiomba serikali itufanyie vipimo kwa mara ya pili ili tuweze kuishi kwa amani hasa katika kipindi hiki ambacho unyanyapaa ni mkubwa kwa jamii," alisema Hamad Khamis (sio jina lake halisi).

Alieleza kuwa licha ya kupata ruhusa ya kutoka hospitali baada ya kupona ugonjwa huo, aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa jitihada zake za kuwagharamia wagonjwa wote ambao walikuwa katika vituo maalum vya wagonjwa wa corona.

Alisema walikuwa wakiishi katika kambi hizo katika hali nzuri na kuwa na uhusiano mzuri kati ya watoa huduma na wagonjwa.

"Kwa kweli wahudumu wa afya wa corona wanastahiki pongezi na pia baada ya kumaliza ugonjwa huu wapewe tuzo maalum kwa sababu walikuwa wakitushughulikia vizuri," alisema.

Alisema katika jambo lolote hakukosi changamoto, awali katika vituo hivyo vya corona kulikuwa na changamoto ya upatikanaji wa chakula kwa wakati, lakini baadaye zikafanyiwa kazi.

Alisema baada ya changamoto kutatuliwa mambo yalikuwa mazuri "tunakula kwa wakati, chakula kizuri tunawapongeza sana viongozi wetu kwa kutujali na kututhamini,"alisema.

Alieleza kuwa walipokuwa vituoni walikuwa na uhuru mzuri ikiwamo wa kutoa maoni yao pale wanapohisi kuwa na changamoto, pia kuruhusiwa kuagiza mahitaji mengine kutoka kwa familia zao iwapo hawajatosheka na chakula kinachotolewa.

Naye mtalamu kutoka Wizara ya Afya ambaye hakupenda kutajwa jina lake, alisema kuwa wagonjwa wote ambao hawana dalili ya corona na kuruhusiwa kutoka hospitali watafuatiliwa na kwenda kupimwa kipimo kwa mara nyingine ili kujua kama virusi vimeondoka.

Kwa upande wake Waziri wa Afya, Hamad Rashid Muhammed, aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo na waliopona corona kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya ikiwamo kujitenga kwa siku 14 kabla ya kufanya shughuli zingine za kijamii.

Jumla ya wagonjwa 36 wameruhusiwa kurejea katika familia zao baada ya kugundulika hawana dalili za corona.




Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Mhandisi Mwanasha Tumbo (aliyevaa hijabu nyeusi), akitoa maelekezo juzi kwa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Frola Kessy ( wa tatu kutoka kushoto), na viongozi wengine, baada ya kupokea msaada wa Matangi mawili ya kuhifadhia maji kutoka kampuni ya Cotex LTD ya jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya watu kunawa maji na sabuni ili kujikinga na Corona katika maeneo ya mikusanyiko ya watu. **PICHA.STEVEN WILLIAM**

# Msalaba Mwekundu yasaidia Magereza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Kimataifa la Msalaba Mwekundu (Red Cross), Kanda ya Zanzibar, limetoa vifaa mbalimbali kwa vyuo vya Mafunzo Zanzibar (Magereza) kwa ajili ya kujilinda na maambukizo ya ugonjwa wa corona ndani ya Magereza.

Mwakilishi wa Shirika la Msalaba mwekundu Zanzibar, Ubwa Salum, alisema wameamuwa kutoa vifaa hivyo kwa Vyuo vya Mafunzo kwa ajili ya kuwalinda wafungwa na watuhumiwa kuwa salama zaidi.

Alisema juhudi za kupambana na ugonjwa huo ni muhimu katika Magereza kwa sababu ukiingia na kuanza kuwashambulia wafungwa na watuhumiwa, unaweza kusababisha maafa makubwa.

"Tumeamua kutoa msaada wetu wenye thamani ya Sh. milioni sita ikiwamo nguo na barakoa pamoja na vitakasa mikono vitumike kwa ajili ya kuwaweka salama wanafunzi wa vyuo vya mafunzo na wafanyakazi wake," alisema.

Naye Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo Zanzibar, Ali Abdalla Ali, aliupongeza uongozi wa Red Cross Zanzibar kwa kutoa msaada huo ambao umekuja katika wakati muafaka wa kupambana na ugonjwa wa corona na kuyafanya Magereza kuwa salama.

Alisema taifa linakabiliwa na mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona na Magereza ni sehemu yenye kuchukuwa na kuingiza watu mbalimbali kwa nyakati tofauti.

Kamishna Ali alizitaja hatua zilizochukuliwa hivi sasa katika kupambana na ugonjwa wa corona kuwa ni kupunguza msongamano katika Magereza na watuhumiwa wanaostahiki kupewa dhamana waruhusiwe.

"Tayari tumeanza kutekeleza agizo hilo la Mahakama Kuu...watuhumiwa wenye sifa ya kupewa dhamana tumewatoa Magerezani ikiwa ni hatua za kupunguza msongamano ndani ya Magereza yetu," alisema.

Kamishna alilipongeza Shirika hilo kwa misaada yake katika nyakati tofauti ikiwa na lengo la kujenga ustawi mzuri katika Magereza nchini.

"Tunalipongeza kwa dhati Shirika la Msalaba Mwekundu kwa msaada wake ambao huu sio wa kwanza...wamekuwa karibu na sisi katika hatua mbalimbali zaidi pale yanapoibuka majanga au magonjwa wamekuwa wakitusaidia," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI MEI 2, 2020



HARRYSONG KWELI AKILI NI BUSARA Uk.14





## UTATA MTUPU

# Mrembo mweusi aichanganya 'Guiness book'

UTATA umeibuka kuhusu habari za mwanamitindo kutoka, Sudan Kusini, Nyakim Gatwechm, maarufu kama 'Queen of the Dark,' kuingia katika kitabu cha rekodi za dunia Guinness, kama binadamu mwenye ngozi nyeusi zaidi duniani.

Mapema wiki hii, mitandao kadhaa na magazeti katika mataifa mbalimbali yamejikuta yakinyooshewa vidole kwa kuripoti habari hiyo inayotajwa kuwa ni ya uongo.

Mtandao wa Standardmedia.co.ke, umejitokeza kukanusha habari hiyo, huku mtandao wa operanewsapp.com, nairaland.com na nanansem.com wakiripoti kuwa mrembo huyo ameingizwa kwenye rekodi katika kitabu hicho.

Nyakim mwenye umri wa miaka 27, anatajwa kuwa ni kivutio katika mitandao ya kijamii, kwa kuwa amekuwa akijitokeza hadharani kufurahia rangi yake hiyo.

Hatua hiyo ya kuingizwa kwenye kitabu cha Guinness, ni kama vile kutuma ujumbe kwa wasichana na wanawake wengi wa kiafrika ambao wanabadilisha rangi za ngozi kwa vipodozi vyenye kemikali kali kuwa weupe,

Katika mitandao kadhaa Nyakim, amekuwa akionyesha furaha na kupiga picha za mapozi ya aina mbalimbali kama ilivyo kwa wanamitindo wengine, hatua ambayo imempa umaarufu na kujikusanyia mashabiki wengi wanaovutiwa msimamo wake huo.

Baadhi ya maandiko kuhusu mrembo huyo katika mitandao kadhaa yanabainisha kuwa, Nyakim Gatwech, huwafundisha watu kutoogopa weusi wa ngozi zao.

"Rangi yangu ni ya kifahari. Ndicho ninachowakilisha, Taifa la mashujaa," ni mojawapo ya ujumbe alioweka katika moja ya picha alizoweka kwenye Instagram.

Akaunti yake inaonyessha kuwa ina wafuasi elfu 10.

Ofisa mtendaji mkuu wa Shear illusions, Shekha Nasser, ambaye ni Mtaalam wa masuala ya urembo, anaeleza jinsi anavyomkubali mrembo huyo kutokana na umakini na utunzaji wa ngozi yake kwa ujumla.

"Anajikubali jinsi alivyo, inaonyesha yupo makini na matumizi ya vipodozi vyake, ngozi yake ina mng'ao mzuri, na unavutia," amesema Shekha.

Mtaalam huyo amesema kutokana na matunzo mazuri ya ngozi yake ni rahisi kumpamba, kumuongezea mvuto kama anavyoonekana kwenye picha zake.

BASI SAWA

## Cheed anapompotezea Harmonize kiaina

MSANII aliyejiengua kutoka lebo ya Kings Music Records Official, Cheed, amesema anaumia kichwa anaposikia uvumi kuwa ana mpango wa kujiunga na Konde Gang, ambayo ipo chini ya msanii Harmonize.

Akizungumza na EATV, Cheed amesema hakuna ukweli katika suala hilo, hata yeye aliona kwenye mitandaoni ya kijamii, jambo ambalo limemzidishia maadui kwa kuanza kutukanwa na mashabiki.

"Hakuna mtu ambaye ametushika akili tutoke Kings Music, ni stori ambazo zinatengenezwa kutokana na hili tukio, suala la sisi kwenda Konde Gang halina ukweli wowote japo hata mimi nalisikia kwenye mitandao.Sasa hivi nashambuliwa kwa kutukanwa sana hadi nazima simu ila mimi nachukulia kama changamoto" ameeleza Cheed.



## Marioo acha utani, kweli huitaki Konde Gang?

MWANAMUZIKI wa Bongofleva, Marioo, amesema imekuwa ngumu kwake kueleza kama atasaini lebo ya Konde Gang, licha ya kufanya kazi na Harmonize.

Akiongea kwenye Friday Night Live ya EATV, Marioo ameweka wazi kuwa tayari amekamilisha ngoma kali na Harmonize, hivyo mashabiki wasubiri kuona mambo mazuri.

''Muda wowote tunatambulisha hilo dude, siku hiyo hakuna kusema kuwa tunatambulisha ngoma bali tunatambulisha muziki, kuhusu kusaini sitasema siwezi au nitasaini, lakini sikuwa na mpango wa kusainiwa na Lebo yoyote maana nina mipango yangu mikubwa'' amesema Marioo.





## Jacqueline Wolper usishangae ya walimwengu

MWIGIZAJI nguli wa Bongo Muvi, Jacqueline Wolper, amesema anapitia changamoto nyingi katika maisha yake, hasa kwenye uhusiano wa kimapenzi kiasi ambacho anapata wakati mgumu kusaidia kazi za wasanii wa kiume.

Wolper amefunguka hayo, kupitia kipindi cha Friday Night Live, ambapo amekiri kuwa kila akiposti kukubali kazi za wasanii wa kiume huwa anapata shida kutokana na watu kuweka mitazamo hasi.

''Unajua inaniharibia sana mpaka natamani kuacha, lakini nimezoea na inabidi tu niendelee na pia mashabiki wanavyonitukana ukifanya jambo fulani inaonekana kama kweli kiasi kwamba mtu unayekuwa naye anakosa imani'' amesema Wolper.

# Makauzu wa Kihindi enzi hizo

**Na Adam Fungamwango**

KWA wale waliokuwa wakipenda kuangaliza filamu za zamani za kibabe, ziwe za kizungu au kihindi, watakuwa wanakumbuka mambo mengi.

Siku si nyingi nyuma tuliangalia filamu za kihindi ambazo zilivuma na kupendwa sana watu kiasi hata cha kuwatoa machozi.

**KABLA YA HUKO**

Leo tutawaangazia waigizaji waliokuwa wakiziweka roho za watazamaji juu, kuanzia mwanzo hadi mwisho wa picha hizo.

Hawa ni wale waigizaji waliokuwa wakiigiza kama maadui kwenye filamu hizo. Walizifanya kazi zao vizuri kiasi cha hata waliokuwa wanaangalia filamu kudhani kuwa hata maisha yao halisi ndiyo walivyo.

**AMRISH PURI 'MZEE ASHANTI'**

Ndiye mwigizaji katili zaidi kwenye filamu nyingi za kihindi. Yeye alikuwa mwigizaji adui anayejulikana, kupendwa na kuchukiwa sana na Wabongo waliokuwa wakiangalia filamu za kihindi wakati huo miaka ya '80 hadi mwanzoni mwa '90.

Watoto na vijana wa Kibongo walimpachika jina la Mzee Ashanti, kiasi cha wengi kutojua hata jina lake halisi. Wengine walimwita 'Mugambo' au 'Adui Kubwa'. Wenyewe wanakwambia picha la kihindi bila Mzee Ashanti halinogi. Anatajwa kuwa ndiye muigizaji katili zaidi kupata kutokea kwenye filamu za kihindi.

Ni mwigizaji aliyejipatia sifa kubwa duniani kutokana na kuigiza kiuhalisia jinsi mtu katili anavyopaswa awe. Na ndiyo maana amekuwa ni mmoja wa waigizaji waliopata tenda ya kuigiza filamu nyingi sana za kihindi wakati huo na nafasi yake ikiwa ni hiyo hiyo ya adui mkuu.

Alifariki mwaka 2005 na kuacha jina kubwa si nchini India tu, bali duniani kote ikiwemo Bongo.

**DANNY DENZONGPA**

Wabongo wanamwita Deni Zompa. Ni mwigizaji mhindi mwenye asili ya Nepal, ambaye naye amejikita zaidi kucheza nafasi ya adui. Ukiacha mzee Ashanti, Deni ni mmoja wa waigizaji katili zaidi kwenye filamu za kihindi, akiwa na uwezo mkubwa wa kuutumia mwili wake kwenye sanaa za mapigano, achilia mbali, silaha mbalimbali. Watoto wa kibongo wakati huo walikuwa wanasema bora ukutane na simba kuliko kuingia kwenye anga za Deni.

**RANJEET**

Huwezi kuwataja maadui kwenye filamu za kihindi bila kumtaja mmoja wa watu waliokuwa wakizifanya zisisimue zaidi wakati huo, aitwaye Ranjeet. Watoto na vijana wakati huo wao walikuwa wakimwita 'Lanjiti'.

Ni mwigizaji katili mwenye roho mbaya, ambaye naye alikuwa akiwaweka roho juu mashabiki wa filamu hizo.

**RAJESH KHANNA**

Ni mmoja wa waigizaji wazuri akicheza kama adui kwenye filamu mbalimbali za kihindi. Pamoja na filamu mbalimbali, lakini unyama wake aliufanya kwenye filamu ya 'Disco Dance' ya Mithun Chakraborty.

**SHAKTI KAPOOR**

Ni mmoja wa waigizaji maarufu wa muda mrefu nchini India ambaye naye huigiza kwenye sehemu za ubabe ubabe, na pia amekuwa akilitendea haki eneo hilo analopangwa kucheza.







## Chid Benzi aanza kuweka 'fiti' umbo

MASHABIKI wa muziki wa Bongo Fleva, wameshindwa kuficha hisia zao baada ya kuona afya ya rapa mkongwe nchini, Chid Benzi, inarudi kama zamani.

Katika kipindi cha wiki moja sasa, mitandao ya kijamii imetawala picha za msanii huyo akionekana na mwili uliojazia na kujaa nuru tofauti na zamani.

Baadhi ya watu ambao waliona picha hizo walichangia maoni yao, wakieleza umbo la sasa ndilo walilozoea kumuona kwani matumizi ya dawa ya kulevya yalimrudisha nyuma na kupoteza dira katika sanaa yake.


Madee au 'Seneda' aliposti picha hiyo katika akaunti yake ya Twitter na kueleza furaha yake baada ya kuona picha ya msanii huyo akionekana wa miraba minne kama anafanya mazoezi ya kujaza misuli.

"Hii ni picha mpya nimeikuta huko mitandaoni. Nafikiri Mungu amezisikia dua zetu, huu ndio mwili ninaoujua mimi toka kwa Chid Benz!!. Mungu azidi kukuongoza bro!!", ameandika Madee.

Picha hiyo ambayo aliiweka kwenye ukurasa wake wa Instagram, Chid Benz aliambatanisha na ujumbe unaosema "kila siku ni siku nasisitiza. Unaweza kuwa vyovyote ukiweza, na ukafanya yote unayoweza. Badilika ili ubadilishe unachowaonesha".

Chid Benz amekuwa na safari ndefu katika muziki wake kwenye miaka ya hivi karibuni, kutokana na mara kadhaa kuonekana akijiingiza katika matumizi ya madawa ya kulevya. Lakini hivi sasa ameonekana kujinasua kwenye janga hilo.

# Furaha iko wapi? Mipango si matumizi




**Na Adam Fungamwango**

WASWAHILI wanasema mipango si matumzi, na kama kitu si riziki basi hakiliki. Hivi ndivyo inawatokea watu kwenye dunia hii. Mtu anaweza kuwa wamepanga kufanya vitu fulani, lakini visifanikiwe kwa sababu mbalimbali za kibidamu au za kiasili.

Filamu ya 'Furaha iko Wapi?' inaonyesha jinsi wakati mwingine inavyofkiria wewe, sivyo inavyotokea.

Imechezwa na wasanii mbalimbali, akiwamo msanii wa bongo fleva, 20 Parcent, Hashim Kambi, Charles Magari, Stanley Msungu na wengine wengi.

Parcent ni mtoto wa kimasikini aliyezaliwa kijijini. Aliishia darasa la nne tu. Maisha yakawa magumu akaamua kwenda mjini Dar es Salaam kutafuta kazi.

Kufika mjini wakati anashangaa maghorofa alipigwa mzinga na gari moja, lakini dereva akawa msamaria mwema, akamchukua na kumpeleka hospitali.

Dereva huyo anaitwa Suzana, binti wa mfanyakazi mwenye wadhifa mkubwa serikalini.

Anamtibia na baada ya hapo, binti anamueleza Parcent jinsi anavyompenda japo yeye ni mtoto wa kitajiri na mwenzake ni masikini. baada ya majadiliano marefu, Parcent anakubali ombi.

Shughuli ndiyo inaanzia hapo. Kijana anaamua kumpeleka binti kwa wazazi wake kijijini kwenda kumtambulisha. Huko anakutana na masharti ya baba yake mzee Magari ambaye anaonekana hamtaki binti huyo, badala yake wanamtaka mmoja wa mabinti kijijini hapo.

Parcent na Suzana wakaondoka kurejea mjini wakiwa wamenyong'onyea. Siku nyingine tena, binti alikwenda kumtambulisha kwao. Huko nako wanakutana na mzee Kambi ambaye ni baba yake Suzana ambaye naye hakukubaliana na binti yake kumletea mchumba fukara na asiyekuwa na elimu.

Hata hivyo mapenzi yao yaliendelea na binti akapatwa ujauzito uliosababisha afukuzwe nyumbani, akamfuata mwenzake ghetto.

Maisha yao yakawa ya tabu kwa sababu wao walipanga hivi, lakini watu wengine wanaowazunguka nao waliwapangia vingine.

Mwanamume akaenda mjini na kumuacha mkewe mjamzito, lakini kutokana na ugumu wa maisha akajikuta akiingia kwenye wizi, akakamatwa na kufungwa, huku mkewe akijifungua bila msaada wowote.



# Mercy akumbuka madhira ya mama

MSHINDI wa shindano la Big Brother Nigeria awamu ya nne, Mercy Eke, amesema mama yake alijaribu kutoa ujauzito kutokana na maneno kutoka ndani ya familia yake.

Akizungumza katika kipindi cha televisheni, Mercey, amesema wakati akiwa tumboni, mama yake aliamua kuitoa baada ya ndugu zake kukataa kumsaidia kulea mtoto.

"Mama aliniambia kwamba, wakati amenibeba mimi tumboni, alipata tabu kutokana na maneno ya familia yake. Walimwambia kwa nini anaendelea kupata ujauzito wakati anao wengi," amesema.



## Stella kumbe ulimnyima penzi mumeo?

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Stella Damus, ameamua kuweka wazi siri ya ndoa yake na mume wake Daniel Ademinokan.

Amesema kabla ya kufunga ndoa yeye na mumeo hawakufanya mapenzi.

Stella amesema ushauri huo ulitolewa na mchungaji wao ambapo mume wake ni mkurugenzi wake katika kazi zake za filamu, alijisikia vibaya kuhusu suala hilo.

## Juliet kwa maneno hayo, amekusikia

MWIGIZAJI kutoka Ghana, Juliet Ibrahim, amempa makavu mpenzi wake wa zamani, Iceberg Slim, asijipendekeze kipindi hiki ambacho yupo kuzuizi cha ndani.

Slim ambaye ni mwanamuziki amekuwa na kawaida ya kumtumia ujumbe kupitia simu ya mkononi na kumletea usumbufu.

"Iceberg Slim, uhusiano wetu uliisha miaka miwili iliyopita kutokana na matatizo yako, bado unatafuta njia ya kunifanya nijifikirie kwa kila wakati," amesema Juliet.





## Kylie hongera kununua hekalu

MJASIRIAMALI bilionea, Kylie Jenner, amefanya kufuru baada ya kununua jumba la kifahari jijini Los Angeles.

Mjengo huo ambao una kila kitu ndani umemgharimu kiasi cha dola milioni 36, katika eneo la Casablanca.

Nyumba hiyo ina upana wa futi 15,350, ikiwa imejengwa kisasa na sehemu kubwa ya bustani inayowawezesha watu kupumzika.

## Harrysong kweli akili ni busara

MWANAMUZIKI Harrysong, ametoa wito kwa Rais wa Nigeria, kuwekeza katika elimu kwa lengo la kuimarisha uchumi uliotetereka.

Akiandika barua ya wazi kwa Rais Buhari, msanii huyo amesema kiongozi huyo lazima atumie akili katika kuinua uchumi ulioyumba kutokana na ugonjwa wa corona.

Amesema kuanzia huduma ya afya, elimu, ulinzi, uongozi na mambo mengine yameparaganyika na kunahitajika nguvu kubwa kurudisha katika hali ya kawaida.



MAKALA

# Athari za kitabaka, jinsia, elimu kusimama wakati wa corona

**Na Michael Eneza**

KUNA hatari ya kupoteza mwaka mmoja katika mtiririko wa elimu kutokana na kuendelea kushamiri kwa homa ya corona, hivyo kulazimisha shule na vyuo kuendelea kufungwa.

Wakati shule zilipofungwa kwa mwezi mmoja kuwezesha serikali kuchukua hatua kadhaa kupambana na kuenea kwa janga hilo, hasa kutokana na kilichotokea nchi za mbali kimsingi wanafunzi walikuwa kama wamepata likizo ya ziada.

Ila kwa muda wote wa ziada ambako likizo hiyo inaendelea, na kulingana na kinachotokea katika familia za watu, zipo athari tarajiwa.

Maisha ya kuwa mwanafunzi kama zilivyo shughuli nyingine kijamii au kifamilia yana maeneo mawili, moja ni matazamio, ambayo hasa ndiyo yanatoa changamoto na hamasa ya kuendelea na maisha hayo, licha ya kuwa na sulubu za hapa na pale. Upande mwingine ni kuvumilia, kuwa bado wakati mfupi tatizo hilo linakwisha na mtu anaanza maisha mapya, awe ni mzazi ambaye mwanae yuko shuleni, au kijana asiye na furaha eneo anapokaa na kusoma, anavumilia tu hali hiyo iishe ili asilete ugomvi endapo ataacha shule mapema. Livu ikiwa ndefu mno, 'anabanjuka.'

Wakati kimsingi kipindi hiki cha vizuizi vya aina tofauti kutokana na corona ni mazingira ambayo kila mtu anatakiwa kuangalia yuko wapi na inabidi akutane na nani, kupungua kwa shughuli za kawaida pia kunaleta uhaba wa riziki katika maeneo mapana tu kijamii. Shughuli za elimu kwa mfano zinaposimama, kuna mlolongo wa wahusika na shughuli hizo siku hadi siku ambao matazamio yao yanaathirika, kwa mfano washona nguo za shule, wasafirishaji wao, iwe ni kwa mabasi maalum au ya kawaida. Nauli zao siyo kubwa lakini zinajazia kwa kiasi si haba.

Kwa mazingira hayo, kupungua kwa vipato kutokana na vizuizi na kukwama kiasi fulani kwa shughuli



tofauti kunaleta athari za utegemezi kuongezeka au kuwa hali ya kawaida kwa wale ambao walikuwa wanajimudu. Ina maana kuwa katika familia ambayo mlezi – awe baba, mama au mhusika mwingine ambaye familia hiyo inamtegea anapokuwa katika mkwamo, athari tanzu zinaanza, kila mtu anatafuta mlango wa kutokea, au njia ya kujikimu. Ni kuingiza uwezo wa kufanya kazi katika soko ambalo tayari limedoda kwa kutokuwapo shughuli za kutosha, hivyo bidhaa ya uwezo wa kufanya kazi inakosa mnunuzi,

**Kutokana na ulazima wa jamii kuendelea kuhakikisha huduma za aina kadhaa zinapatikana, vinginevyo hata uhai wenyewe unakuwa mashakani, mikwamo hii ya kifamilia itaathiri zaidi wanafunzi, na hasa watoto wa kike**

inabaki tu hitaji la kawaida, lipangiwe pesa.


Kutokana na ulazima wa jamii kuendelea kuhakikisha huduma za aina kadhaa zinapatikana, vinginevyo hata uhai wenyewe unakuwa mashakani, mikwamo hii ya kifamilia itaathiri zaidi wanafunzi, na hasa watoto wa kike. Pale walipokuwa wamesimama kidete kufuatia masomo yao hadi yakamilike na kutazamia labda kuendelea zaidi siku za usoni, ngoja isiyo na mwisho inabadili hali hiyo.

Walio katika familia zinazojiweza ambako hakuna manyanyaso mapya kutokana na mikwamo ya corona, ambako mtoto wa kike atajihisi anathaminiwa kama ilivyo kawaida, hapawezi kuwa na athari za wazi. Ni pale mtoto akionekana mzigo kwa sababu mzazi au mlezi amekwama ndiyo hapo athari zinaweza kutokea, kwani ni msambaratiko wa kifamilia.

Taarifa zinazotoka nchi kadhaa ambako uzururaji wa watu nyumbani umesimamiwa kwa nguvu na vyombo vya dola kupunguza kasi ya maambukizo ya corona zinaonyesha kuwa udhaifu wa kifamilia na hata kuvunjika kwa amani kunaongezwa na hali ya kutotoka nyumbani. Imefikia mahali ambapo Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, aliona azungumzie suala hilo mwenyewe, hali ya zuio la watu kubaki nyumbani. Imeongeza kwa kasi kubwa mifarakano.

Ni rahisi kuelewa hali hiyo kwani watu wengi wanaishi kwa kutegeana, kuondoka asubuhi na kurudi jioni au usiku kila mtu amechoka wanalala, hakuna wakati wa mazungumzo mengi na kukumbushana machungu. Ni katika hali hiyo ambako mwanafunzi aliyekuwa akingoja mwaka uishe aanze maisha mengine, iwe ni kwa kufaulu au kupata cheti atafute kazi, au angalau awe huru kujiamulia hali yake ya baadaye bila kubanwa na sheria, atakapoanza kuchoshwa na ngoja ya corona. Halafu haina mpaka kuwa mwezi huu au ujao au hadi Oktoba itakuwa imekwisha.

Kwa maana hiyo kuna hitilafu ya uvumilivu inayoweza kutokea, kuwa mwanafunzi akiona shule hazifunguliwi na nyumbani hapakaliki, siyo rahisi kuendelea kuvumilia. Ni suala la utafiti ni njia gani zinaweza kutumika kumtenganisha na nyumbani endapo anaweza akafanya vingine, ingawa hali hiyo bado haijawakuta wengi, kwani bado ni mapema tangu shule zimefungulia. Kimsingi ni kuwa siyo kila mwanafunzi atarudi shuleni zikifunguliwa, na kama itapita miezi kadhaa au hata kukaribia mwaka, wengi tu watakuwa wamebadili mazingira, siyo lazima kuwa yatakuwa bora zaidi bali wanaweza kuwa huru zaidi, kwani la msingi katika maisha ni riziki tu.



Ushauri unaotolewa na wataalamu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu namna ya kukaa katika mazingira ya kizuizi, kuhakikisha afya kiakili na kimwili ni wazi unawafaa zaidi walio na mazingira mazuri ambayo hayategemei shughuli za kila siku kupata riziki. Wale ambao kukaa ndani kunavuruga vipato ni kazi ngumu kubakiza akili mahali pamoja na kuelekeza mawazo katika vitu kama televisheni, vitabu au hata maombi kwani kwa Afrika suala hilo ni muhimu, ingawa ng'ambo si rahisi likatajwa au kuona limezoeleka. Ugumu wa maisha unapunguza utashi wa kukaa pamoja, na uanafunzi bila shule unageuka u-house girl au kuwa mzigo kwa ndugu, hivyo haitakuwa vigumu kuvumilia. Ni kukatisha masomo endapo shule hazifunguliwi mapema.

COVID 19

# Wanaume wapo hatarini zaidi kuliko wanawake



Rais wa Slovakia , Suzana Caputova, akiwa amevaa barakoa pamoja na wasaidizi wake. . **PICHA NA MTANDAO**

**Na mwandishi wetu**

KUNA jambo la kushangaza kuhusu ugonjwa wa COFID 19, nalo ni kitendo cha virusi vya corona kuwaathiri zaidi wanaume kuliko wanawake.

Katika utafiti uliofanywa umegundua mpaka Aprili 7 mwaka huu, jumla ya wanaume 2,232 walifariki kutokana na virusi hivyo katika jiji la New York, Marekani, wakati wanawake walikuwa 1,309.

Hata kwa wagonjwa waliolazwa kwenye hospitali mbalimbali nchini humo, wanaume ni 40,000 na wanawake 34,000.

Katika ripoti hiyo kiwango cha vifo vya Covid 19 miongoni mwa watu 100,000, wanaume ni 55, chini ya wanawake wanaofikia 30.

Wanaume wengi wamekutwa na ugonjwa wanaonekana kupata athari mbaya ya kiafya.

Idadi ya vifo miongoni mwa wanaume inaonekana kuwa kubwa katika kila umri kuliko wanawake.


"Suala hili linafaa kutuamsha ili kuendelea kuwalinda wenzetu walio katika vyumba vya uuguzi", alisema Birx wakati alipokuwa akitoa habari kwa jopo la Rais Donald Trump la kupambana na virusi vya corona.

Utafiti wa hivi karibuni uliofanywa nje ya China, ulibaini kwamba kiwango cha vifo miongoni mwa wanaume ni asilimia 2.8 ikilinganishwa na asilimia 1.7 ya wanawake.

Uchanganuzi mwingine uliofanywa nchini China ulibaini kwamba kati ya watu waliofariki na virusi hivyo asilimia 60 walikuwa wanaume.

Nchini Italia ripoti ya vifo inaonyesha asilimia 72 ya wale waliofariki walikuwa wanaume. Utafiti mwingine uliiweka idadi hiyo kuwa zaidi ya asilimia 80.

Wataalam wametoa sababu kadhaa ambazo zinaweza kuelezea tofauti hiyo, ikiwamo mfumo wa kinga kati ya wanaume na wanawake kuwa tofauti, mitindo ya maisha na uwezekano wa wanaume kujiweka katika hatari nyingi.



Kirusi cha corona kikiwa ndani ya mwili

Kwa mfano, wanaume wana uwezekano wa kuvuta sigara, huku asilimia 40 wakitumia bidhaa hiyo duniani ikilinganishwa na asilimia 9 ya wanawake, kulingana na shirika la afya duniani (WHO) linawaweka katika hatari kubwa ya kukutwa na magonjwa ya mapafu.

Wanaume pia hunywa pombe nyingi na mara nyengine hukataa kwenda hospitali wakati wanapokuwa katika hali mbaya ya kiafya.

Wakati huohuo wanawake wana uwezo mkubwa wa kukabiliana na maambukizo ya virusi ikilinganishwa na wanaume

"Kuna kitu kuhusu mfumo wa kinga ya wanawake kuwa imara zaidi," Dk Janine Clayton, mkurugenzi wa Ofisi ya Utafiti juu ya Afya ya Wanawake katika Taasisi za Afya za kitaifa, aliiambia New York Times.

Wanawake pia wana nafasi nzuri ya kinga kwa kumiliki kromosomu mbili za X , ambazo zinaweza kuchangia katika kuimarisha kinga wanapokabiliana na maambukizo ya virusi .

"Baadhi ya sababu zisizojulikana kwa nini Covid-19 huenda ni hatari zaidi kwa wanaume zaidi ya wanawake ni kwamba ugonjwa wa moyo hupatikana sana miongoni mwa wanaume wenye umri mkubwa zaidi ya wanawake", anasema Dkt Stephen Berger, mtaalam wa magonjwa ya maambukizo na mwanzilishi mwenza wa shirika la Global Infectious Diseases and Epidemiology Network (GIDEON).

Tafiti pia zimebaini kwamba shinikizo la juu la damu na magonjwa ya ini hupatikana sana miongoni mwa wanaume, suala linalochangia vifo vya Covid-19.

Kutokana na hali hiyo, Marekani iliamua kuzindua matibabu maalum kwa wanaume.

Katika vipino hivyo, wanasayansi wanawapatia wanaume walio na COVID-19 homoni za kike ili kuona iwapo zinaweza kuwasaidia kupona Covid-19.

**IDADI KUONGEZEKA DUNIANI**

Wakati utafiti huo ukionyesha wanaume wako hatarini zaidi, wasiwasi unazidi baada ya kufahamika kwamba, huenda watu bilioni moja wakaambukizwa virusi vya corona duniani kote.

Hata hivyo, nchi masikini zinahitaji misaada ya haraka kukabiliana na ongezeko hilo.

Kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Kutoa Misaada (IRC), limesema misaada ya kifedha na kibinadamu inahitajika kupunguza kasi ya usambaaji wa virusi vya corona.

Shirika hilo limesema nchi zinazokabiliwa na vita kama Afghanistan na Syria zinahitaji msaada wa dharura kuzuia mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Kumekuwa na zaidi ya watu milioni 3 walioambukizwa ugonjwa wa Covid-19 duniani, huku watu 200,000 wamefariki.

Ripoti ya shirika hilo, ambazo zinatokana na Shirika la Afya Duniani (WHO) na chuo cha Imperial College cha London Uingereza, ilikadiria kwamba kunaweza kuwa na maambukizo kati ya milioni 500 na bilioni 1 katika kipindi kifupi.

Pia imesema kwamba huenda idadi ya vifo ikafikia milioni tatu katika nchi zinazokumbwa na migogoro na zisizokuwa na uthabiti.

"Idadi hiyo inastahili kutufungua macho," amesema mkuu wa shirika la IRC, David Miliband.

Anaongeza kusema "Maafa ya janga hili bado hayajashuhudiwa sana katika nchi zilizoathirika na vita, jambo la msingi sasa ni kwa wafadhili kutenga pesa kwa mataifa hayo.Serikali zinastahili kushirikiana kuondoa kizuizi chochote dhidi ya msaada wa kibinadamu,"

**Kwa msaada wa mitandao**

## HABARI KIMATAIFA

# Donald Trump atofautiana na majasusi kuhusu corona

**WASHINGTON,** Marekani

MVUTANO umeibuka kati ya Rais wa Marekani, Donald Trump, na Idara ya Intelijensia ya nchi hiyo, kuhusu chanzo cha virusi vya corona.

Wakati Trump anadai kuwa ana ushahidi virusi vya COVID 19 vilitengenezwa katika maabara moja ya China, ofisi ya mkurugenzi wa shirika la ujasusi la nchi hiyo, alisema bado inachunguza chanzo cha virusi hivyo.

Katika taarifa yake, ofisi hiyo ilisema kuwa haijabaini ikiwa Covid-19 ilitengenezwa na binadamu au kupitia mfumo wa maabara.

Hata hivyo, China imepinga madai ya Trump, virusi hivyo vilitengenezwa katika maabara yake mjini Wuhan ambako ugonjwa huo ulianzia.

Akihutubia waandishi wa habari Ikulu ya White House, Trump alisema hayo wakati akijibu swali aliloulizwa kama ana uhakika Taasisi ya Virology ya Wahun, ilikuwa chimbuko la virusi vya corona.

"Ndio, nina hakika. Ndio, nina hakika," alisema Trump, aliongeza kufafanua "Siwezi kuwaambia jambo hilo. Siruhusiwi kusema suala hilo."

Alihoji kama China walifanya hivyo bila kukusudia au walikosea na kutengeneza nyingine?

"Hata mimi sielewi ni kwa nini watu hawaruhusiwi kwenda kupumzika China lakini wanaruhusiwa katika maeneo mengine ya dunia. Jambo hilo ni baya na swali gumu kwa wao kujibu." Alisema Trump.

Gazeti la New York Times, siku ya Alhamisi liliripoti kuwa maofisa wa ngazi ya juu wa Ikulu, waliomba Marekani kuchunguza kama virusi vimetokea katika maabara ya utafiti ya Wuhan.

Shirika hilo la ujajuzi limetakiwa kuthibitisha kama China na Shirika la Afya Duniani (WHO), linaficha taarifa za awali ya virusi vya corona.

Ofisa wa Mkurugenzi wa Taifa wa Intelijensia, akijibu kauli hiyo alisema wamechunguza kwa kina na kuungana na wanasayansi wengine kwamba ugonjwa wa Covid-19 chanzo chake ni cha asilia.

"Jumuiya ya intelijensia itaendelea kuchunguza taarifa za chanzo cha ugonjwa huu kama maambukizi yalianzia kwa wanyama au ni matokeo ya ajali ya kisayansi katika maabara ya Wuhan." Ilisema taarifa hiyo.

Hivi karibuni, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, aliitaka China kukubali wataalamu kutoka nje kuchunguza eneo hilo kwa ajili kujiridhisha usalama wa maabara zake na sehemu nyingine za nchi hiyo.

China ilikataa wito huo, ikisema madai hayo hayana ushaidi wowote na hayajengi.

Lakini pia wanahusisha na hasira za Marekani kudai kuwa serikali ya China haikutoa na takwimu za kweli kuhusu mlipuko huo unavyoanza.

**BBC**




Mji wa kale wa Edinburgh, Uingereza, ukionekana ukiwa tupu wakati watu wakiendelea kukaa ndani kutekeleza amri ya kutotoka nje kwa ajili ya kupambana na virusi vya corona. **PICHA: THE TIMES**

## Waziri Mkuu Urusi augua COVID19

**MOSCOW, Urusi**

WAZIRI Mkuu wa Urusi, Mikhail Mishustin, ametangaza kuambukizwa virusi vya COVID 19 na tayari amemfahamisha Rais Vladimir Putin, kuhusu afya yake.

Mishustin, alisema amejiweka karantini nyumbani kwake kwa ajili ya kuangalia maendeleo ya afya yake.

Urusi ina wagonjwa wa corona 106,000 na nusu yake wametokea mji wa Moscow.

Meya wa mji huo amesema hafikirii kwamba mji huo mkuu umekaribia kuvitokomeza virusi hivyo.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, ambaye amepona ugonjwa huo, alisema nchi yake imevuka salama kilele cha hatari kutokana na mripuko wa virusi vya corona.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa mara ya kwanza tangu aliporejea ofisini, Johnson, alisema atawasilisha mpango kabambe wiki ijayo kuhusu lini na vipi Uingereza italegeza masharti yaliyowekwa ya kupambana na virusi vya corona.

DW

## Mei Mosi yaathiriwa na corona

**HONG KONG, China**

WAFANYAKAZI wa Hong Kong, waliojaribu kuandamana katika maadhimisho ya siku ya kimataifa ya wafanyakazi, Mei Mosi, wametawanywa kuhofia kuenea kwa virusi vya corona. Hata hivyo baadhi yao ambao walivalia barakoa, walielekea mitaani huku wengine wakielezea hisia zao kupitia mitandao ya kijamii.

Kwa kawaida inapofika tarehe hiyo, mamilioni ya wafanyakazi hujitokeza kuandamana na kusikiliza hutuba mbalimbali za viongozi.

Lakini kufuatia masharti ya watu kukaa mbali na mwingine, utamaduni huo haukuwepo katika miji mingi.

DW

# Rwanda, Afrika Kusini zalegeza masharti

**Kigali, Rwanda**

BAADHI ya nchi za Afrika, ambazo zilichukua hatua kali kudhibiti maambukizo ya virusi vya Corona, zimeanza kulegeza baada ya kupungua kwa kasi ya visa vya ugonjwa huo.

Rwanda inatarajiwa kutoa tangazo la kupunguza masharti kwa kuwaruhusu watu kutoka nje na kufungua shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Tangazo hilo linaeleza hatua hiyo itaanza siku ya Jumatatu, ambapo watu wataruhusiwa kurudi kwenye biashara zao binafsi, kufunguliwa ofisi za umma na kuacha masharti kidogo yakifanya kazi.

Mpaka sasa nchi hiyo imeripotiwa kuwa na wagonjwa 243, maambukizo mapya yakiwa ni watu 84 ambayo yaliripotiwa siku saba zilizopita. Waziri wa afya wa nchini humo anasema idadi hiyo ya maambukizo inaongezeka kwa sababu ya kuruhusu madereva wa maroli kuingia kutoka Kenya na Tanzania.

Maeneo yatakayoruhusiwa ni masoko yatakayofunguliwa kwa wauzaji asilimia hamsini, hoteli na migahawa zitarejea na kufungwa saa moja usiku.

Sehemu za michezo, mazoezi, vilabu vya pombe na nyumba za ibada zitaendelea kufungwa.

Pia shule zote zitaendelea kufungwa mpaka mwezi Septemba 2020, na mipaka yote itafungwa isipokuwa kwa malori ya mizigo.

Kwa upande wake Afrika Kusini, jana ilianza kutekeleza masharti mapya yaliyowekwa na serikali baada ya wiki tano ya vizuizi vya kutotoka nje.

Katika utaratibu huo, baadhi ya biashara zitaruhusiwa ikiwa ni pamoja na mikahawa ya chakula na watu kutoka nje ya nyumba zao. Hata hivyo, serikali ilisisitiza itawapeleka polisi kulinda usalama mitaani.

**BBC**

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini- 10

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

**Na Adam Fungamwango**

"Wala tusipepese macho hapa. Ili mali kisheria irudi kwetu ni lazima Shani asiwepo. Yeye ndiyo pingamizi pekee la kisheria kwetu. Patiyo angekuwa na watoto watatu wanne au zaidi tungesema warithi ni wengi. Lakini hapa jinsi ilivyo ni kwamba wazazi wa marehemu ambao ni wazazi wetu pia wamefariki. Marehemu amefariki huku mkewe pia akiwa ameshafariki siku nyingi na hata huyu aliyemuoa tena wameuawa wote kwa pamoja. Hana watoto wengi ana mtoto mmoja tu. Kama hayupo huyu Shani, kisheria ni kwamba mali inarudi kwa ndugu wa baba na mama mmoja. Ni Shani pekee ndiye anayeleta uzito hapa." Ben alizidi kuwafafanulia wenzake jinsi sheria inavyofanya kazi yake.

"Sasa tunafanyaje?" Paul aliuliza wenzake.

"Hapa ni kwamba Shani asiwepo tu. Yeye ndiye kipingamizi kwetu." Jim alitoa ushauri wake.

"Aende wapi sasa." George aliuliza.

"Mimi naona tumuendee kwa mganga, amroge awe mwendawazimu. Nadhani hii pekee inaweza kutufanya tukusanye mali ya ndugu yetu irudi kwenye ukoo wake." Ben alisema akiwaangalia wenzake na tabasamu juu.

Kicheko kikali kilisikika kutoka kwa Jim, akisha akapanua kinywa chake.

"Ben, yaani wewe mdogo wangu msomi mzima unawaza mambo ya kishirikina!" Akatikisa kichwa kukataa mpango huo.

"Tumtafute mganga, tupate gharama kubwa, amroge, halafu tukae siku kibao na kusubiri ni lini ataanza kuwa chizi, halafu akianza ndiyo twende mahakamani. We hujui kuwa jamii yote inaweza kutufikiria kuwa sisi tumehusika na jambo hilo?" Ben alitoa hoja kukataa mpango huo na kutoa ushauri wake.

"Mimi nafikiria kitu kimoja tu cha kufanya. Auawe. Akiuawa hakutakuwa na kipingamizi tena. Mali itakuwa yetu sisi wanne na tutagawana sawa bin sawia."

"Anauawa vipi?" George alizidi kudadisi.

"Ni mchezo mdogo tu ndugu zanguni. Wala sisi hatumgusi. Tunaweza kukodisha mtu ammalize tu kwa risasi." Jim aliwaeleza ndugu zake.

"Mimi nina wazo." Paul alidakia. "Mimi naona tusimpige kwa risasi, maana huyu ni damu yetu. Ni mtoto wa kaka yetu. Pamoja na kwamba tunataka mali, lakini tuangalie utu vile vile, nafikiri tumuwekee sumu kwenye chakula itakayomuua taratibu. Nafikiri iikae kwa muda wa wiki moja ndiyo afe." Paul alisema na kumfanya kaka yake Jim atikise kichwa.

"Hapo umesema ndugu yangu. Ila ujue kufa ni kufa tu, lakini hii mbinu itatuweka salama zaidi. Akifa na sumu ambayo ikionekana imewekwa kwenye chakula, hakuna atakayetufikiria sisi kwa sababu sisi siyo wapishi wala hatuhusiki na mambo yake binafsi hasa ya chakula, ila kama angeuawa kwa risasi, ingeonekena tumekula njama." Jim alipigilia msumari kuwa mbinu ya kumuwekea sumu kwenye chakula inafaa sana.

"Mpango wote, nani ataifanya kazi hiyo, wapi, niachieni mimi, ila ushauri unatakiwa nini cha kufanya kwa sababu chochote kinaweza kubadilika muda wowote sawa?" Jim alisema na kufunga kikao.

===============================

Ndege kubwa iliwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam. Ilikuwa ni Shirika moja kubwa la ndege la Uarabuni. Ndege ilitoka nchini Marekani kupitia Ufaransa mpaka nchini Tanzania.

Jumla ya abiria 200 walikuwa wameteremka ndani ya ndege hiyo. Baadhi walikuja kuchukuliwa na ndugu zao, lakini baadhi walionekana ni kama wenyeji tu katika jiji la Dar es Salaam.

Eddy Kamal, alikuwa mmoja wa abiria hao. Alikuwa amevaa jinzi ya kubana na iliyopauka. Chini alivaa kiatu vyepesi, halafu juu alikuwa amevaa fulana ya kijivu ya mikono mirefu. Alivaa mawani ya jua na alionekana ni mmoja wa abiria wa kawaida ambao hawakumvutia mtu yoyote uwanjani hapo.

Alikuwa na kibegi kidogo mgongoni. Alionekana kabisa ni mmoja wa abiria ambao ni wenyeji kwenye jiji la Dar es Salaam, kwani alitoka mwenyewe baada ya kukamilisha taratibu zote, akaenda moja kwa moja hadi zinakopaki taxi. Akasalimiana na mmoja na dereva na kuingia ndani ya gari.

"Nipeleke Kijitonyama." Alisema abiria hiyo. Dereva akatii amri na kuondoa gari, ikianza kutafuna lami kuelekea ilikotakiwa iende.

Alikuwa nje ya Tanzania kwa muda wa mwaka mmoja. Alikwenda nchini Marekani kuongeza ujuzi wa mambo ya intelejensia.

Ni mfanyakazi wa Idara ya Usalama ambaye mara nyingi amekuwa msaada mkubwa wa taifa, na hasa uwezo wake na kung'amua na kuvumbua uhalifu, au hujuma kwa taifa na kupambana nalo, kabla hasara au maafa hayajatokea.

Ameshawahi kufichua njama za wapigaji, wahujumu uchumi na mafisadi na hata wakwepa kodi sugu, kitu ambacho kimemfanya kupendwa mno na mabosi wake na hata taifa kwa ujumla.

Mbali na hilo, ameshawahi kupeleleza na kufichua baadhi ya visa na mauaji ambayo awali yalionekana ni ya kawaida tu, lakini kunbe yalibeba mambo mazito nyuma ya pazia.

Eddy, kijana mwenye miaka 35 tu, muonekano wake wa nje ni kijana mrefu mwembamba, mwenye uso wenye haya mpole na mchanganfu pia. Huongea taratibu na kwa makini, hasa anapokuwa kazini au kwa mtu asiyemfahamu.

Kinyume chake ni hatari kuliko Simba. Ni mmoja wa wapelelezi makini, mwenye kipaji cha hali ya juu nchini.

Amekuwa akiingia na kupeleleza matukio tata ambayo awali hayakuwa na ushahidi hata chembe, lakini amekuwa akizama na kutoka na jawabu, pamoja na ushahidi.

Mambo mengine yaliwashangaza hata mabosi wake, kwani kesi zingine huwa zimejisokota na inakuwa ni ngumu kupata ushahidi, lakini pia ilibidi ahatarishe maisha yake na mara nyingi amekuwa akiponea chupuchupu kuuawa na watu ambao hawaitakii mema nchi, lakini mara zote amekuwa akiwashinda katika namna ya ajabu na kuibuka shujaa.

Ndiyo maana ilipokuja nafasi ya kwenda kuongeza ujuzi nchini Marekani, mabosi wake kwa kauli moja, walipeleka jina la Eddy Kamal serikalini.

Kitu kingine ambacho mara kwa mara humfanya mshindi, pamoja na uwezo wa kunusa uhalifu, lakini pia ni uwezo wake kwenye sanaa za mapigano.

Hakuwa na mwili mkubwa, lakini ulijaa mafunzo ambayo awali, zaidi ya miaka 10 iliyopita aliyapata kutoka nchini China, lakini pia alikwenda nchini Cuba kwenye mafunzo ya kutumia silaha, lakini pia kukabiliana na maadui wenye silaha.

Nchini Marekani alikwenda kuongeza ujuzi kama huo, lakini kwa sasa ukiboreshwa na mbinu za kisasa zaidi, pamoja na kutumia teknolojia zinazoendana na wakati.

Mita kadhaa ya kutoka nyumbani kwake, alisimamisha gari na kumlipa pesa dereva akateremka na kumuaga.

Mara nyingi watu wa ina hii huishi kwa kanuni zao. Hawana tabia ya kuishi kama watu wa kawaida tu.

Ingekuwa mtu wa kawaida basi dereva angeambiwa afika nyumbani, amshushe mlangoni au getini.

Hakuwa na wasiwasi sana na nyumbani kwake, kwani usalama, uangalizi na usafi wote aliuacha kwa watu wa ofisi yake.

Baada ya ziara ya nyumba yake aliyoiacha mwaka mmoja uliopita na kuona kila kitu kiko sawa, aliamua ajipumzishe kutokana na safari ndefu ya zaidi ya masaa 24.

Alijua siku tatu baada ya kutua nchini anatakiwa kwenda kuripoti ofisini. Alitaka kuzitumia siku tatu hizi kuwasiliana na kukutana na ndugu zake, kabla hajaanza kazi. Anajua kabisa kuwa kazi zao huwa haziaminiki.

Kingine kilichomjia kichwani ni kwenda kuzuru kaburi la shangazi yake.

"Ndiyo. Kabla ya kuanza kazi nitakwenda kuzuru kwenye kaburi la shangazi." Aliwaza.

Kifo cha shangazi yake kilimkuta wakati akiwa nchini Marekani akimalizia mitihani yake.

Aliumia mno, kwa sababu alikuwa ni wa mwisho kuzaliwa kutoka kwenye ukoo wa baba yake.

Alikuwa mmoja wa shangazi zake ambaye anaelewana naye sana. Labda kwa sababu wote walikuwa vijana.

Hata hivyo kilichomuuma zaidi ni jinsi alivyokufa. Pamoja na kwamba kifo ni lazima binadamu na mwanadamu aliyezaliwa ipo siku atakufa, lakini kifo cha shangazi yake kilimshangaza na kumshtusha kwa wakati mmoja.

Kitu kimoja tu ambacho kilikuwa kwenye akili yake ni kwamba shangazi yake hakufa kifo cha kawaida. Haikuwa mapenzi ya Mungu.




**Eddy Kamal, alikuwa mmoja wa abiria hao. Alikuwa amevaa jinzi ya kubana na iliyopauka. Chini alivaa kiatu vyepesi, halafu juu alikuwa amevaa fulana ya kijivu ya mikono mirefu. Alivaa mawani ya jua na alionekana ni mmoja wa abiria wa kawaida ambao hawakumvutia mtu yoyote uwanjani hapo.**

ITAENDELEA JUMAMOSI

## Chadema walikimbia Bunge

INATOKA UK.2

limejadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake, na wizara za Tamisemi, Utumishi na Utawala Bora na Muungano na Mazingira.

Nyingine ni Wizara ya Madini, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Maji na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Zilizobaki ni Wizari ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Nishati, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, na kumalizia Wizara ya Fedha na Mipango kabla ya kujadili na kupitisha bajeti kuu ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Wakati Bunge la Bajeti linaendelea jijini hapa, tayari kuna vifo vya wabunge watatu vilivyotokea ndani ya wiki mbili, ambao ni aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Morogoro (CCM), Mchungaji Getrude Rwakatare aliyefariki Aprili 20, mwaka huu na Mbunge wa Sumve (CCM), Richard Ndassa, aliyefariki Aprili 28, mwaka huu.

Wa tatu ni Balozi Mahiga ambaye pia ni Waziri wa kwanza na mbunge wa tisa kwa Bunge la 11 lililoanza mwaka Novemba 2015. Hakuna taarifa iliyotolewa na mamlaka za serikali ikieleza kama vifo vya wabunge hao watatu vilisababishwa na virusi vya corona.

# JPM, mabalozi, wabunge

INATOKA UK.2

Mahiga, alikuwa rafiki mkubwa na aliyekubalika na wanadiplomasia wa kifaransa, akiwa pia ni mjumbe mwakilishi wa kudumu wa Umoja wa Mataifa, daraja kati ya Magharibi na Afrika, atakumbukwa kama mfano kwa kizazi cha sasa cha wanadiplomasia."

Balozi wa Canada nchini, Pamela O'Donnel, alisema: "Salamu zangu za rambirambi ni kwa marafiki na familia ya Balozi Mahiga. Aliwakilisha nchi yake ikiwamo Canada kwa uadilifu na uaminifu mkubwa, kwa kweli tutamkosa."

Katika ukurasa wa Twitter wa Umoja wa Mataifa Tanzania waliandika: "Tunaungana na Tanzania kuomboleza kifo cha Balozi Mahiga. Alikuwa rafiki mzuri wa Umoja wa Mataifa Tanzania (UN Tz) na UN kidunia akifanya kazi kama mwakilishi maalum wa Katibu Mkuu wa UN Somalia."

Balozi wa Ireland, Paul Sherlock, alisema: "Nimepokea kwa mshituko taarifa za kifo cha rafiki yetu nzuri Balozi Mahiga, natoa salamu za rambirambi kwa familia na Watanzania, apumzike kwa amani."

Mwakilishi Mkazi wa UN Tanzania, Zlatan Milisic, aliandika katika ukurasa wake wa Twitter: "UN Tanzania inatuma salamu za rambirambi kwa familia ya Balozi Mahiga, serikali na Watanzania kwa kumpoteza mtu muhimu. Balozi Mahiga alikuwa sehemu ya UN akiwa mwandamizi wa nafasi za juu UN katika nchi tofauti."

Katika ukurasa wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF) waliandika: "Mheshimiwa Mahiga alikuwa kiongozi wa kampeni ya mabadiliko kwa watoto na alitekeleza wajibu mkubwa kusaidia usajili wa watoto wanaozaliwa, UNICEF inatoa salamu za rambirambi kwa familia, serikali na Watanzania."

Ubalozi wa China uliandika: "Ubalozi wa China Tanzania tunaungana na Watanzania kueleza masikitiko yetu kwa kumpoteza Mahiga, mchango wake wenye thamani kwa maendeleo ya uhusiano baina ya China na Tanzania utakumbukwa."

Ubalozi wa Ujerumani nchini ulisema: "Tumeshtushwa na taarifa za kifo ambacho hakikutarajiwa cha Dk. Mahiga. Mtu mahiri na mwanadiplomasia mbobevu, Ujerumani imepoteza rafiki, tunatoa pole kwa familia yake."

Naye Mbunge wa Kigoma Mjini (ACT-Wazalendo), Zitto Kabwe, alisema Balozi Mahiga, aliyezaliwa Agosti 28, 1945, alikuwa mzee mwenye maarifa mengi.

"Ni mtu ambaye nilikuwa nikiwa na jambo linalohusu usalama wa kimataifa, namtafuta kwa ushauri. Ni hazina kubwa Tanzania imepoteza, Namwombea kwa mola aiweke roho yake mahala pema peponi," alisema.



Mafundi wakiifanyia ukarabati barabara ya Umoja wa Mataifa, kutokana na kuharibika katika eneo la Upanga Magharibi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yasisitiza kutoingilia bei ya mazao

**Na Mathias Canal,** DODOMA

SERIKALI imesisitiza kuwa haitopanga wala kuingilia bei za mazao ya wakulima nchini badala yake watajipangia bei na kuuza yenyewe ikibaki kuwa msimamizi.

Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na viongozi wa Tadcos Co ltd kuhusu hatua iliyofikiwa ya uagizaji wa mbolea, jijini Dodoma.

Mgumba alisema mfumo wa biashara ulivyo unategemea zaidi ujazo wa mazao sokoni, hivyo bei haitolewi kutokana na gharama alizotumia mkulima wakati wa uzalishaji badala yake inaendana na soko.

Alisema wakulima kama wanavyoruhusiwa kuzalisha, watauza mazao yao popote watakapotaka lakini kwa kufuata taratibu na sheria za nchi.

Kuhusu mfumo wa stakabadhi ghalani, Mgumba alisema mfumo huo ulianzishwa kwa lengo la kumrahisishia huduma za biashara mkulima hivyo utaendelea kutumika kwa mujibu wa matakwa ya kuanzishwa kwake.

Alisema zipo changamoto nyingi katika utekelezaji wa mfumo huo unaochagizwa na viongozi wanaosimamia hususani wa vyama vya ushirika kutotekeleza kwa mujibu wa sheria.

"Mtu akipeleka mazao yake ghalani lengo la serikali kwa sababu mazao yote tunategemea msimu wa mvua na upatikanaji wake ni wa wakati mmoja hivyo kuhifadhi kwa pamoja na kupewa stakabadhi itakayomrahisishia kupata mkopo kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake wakati akisubiri gharama za mazao zikipanda aweze kuuza kwa bei nzuri," alisema.

Alisema mfumo huo ni mzuri endapo utaendelea kusimamiwa vizuri ikiwa ni pamoja na kuendelea kuuboresha zaidi ili uwanufaishe wakulima kote nchini kwa kuwa mfumo huo unapunguza gharama za uendeshaji.

Alisema miongoni mwa changamoto waliyokuwa nayo wakulima ilikuwa ni tija ndogo katika mavuno yao yaliyosababishwa na matumizi madogo ya mbolea hivyo serikali ilitoa elimu ya kutosha kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya mbolea na katika kipindi cha serikali ya awamu ya tano tija imeongezeka.

Mgumba alisema matumizi sahihi ya mbolea yameongeza tija katika sekta ya kilimo kwa kuwa uzalishaji umeongezeka na wakulima wamekuwa na kipato kikubwa.

Katika kikao kazi hicho Mgumba alisema nchi ina mbolea ya kutosha na akiba ya zaidi ya tani 203,000 iliyotokana na uagizaji wa mbolea uliofanywa kwa mwaka mzima wa kiasi cha tani 633,197.

## Serikali yaondoa kodi kwa vifaa tiba corona

INATOKA UK.4

huu.

"Tunafanya jitihada kubwa timu ya kitaaluma inachambua taarifa za kila sekta, kuangalia athari ni nini na nini kifanyike ili tukabiliane na corona. Hizi za kisekta zinahitaji uamuzi wa jumla wa serikali kama kuahirisha matumizi ya baadhi ya maeneo na kuna miradi ya maendeleo ambayo haijaanza kabisa," alifafanua.

Waziri Mpango alisema wanatarajia kutoa unafuu wa kodi kwa biashara ambazo zitaathirika na kurefusha muda wa marejesho ya mikopo na kuipitia upya ili kuwasaidia Watanzania.

"Serikali inakamilisha mkakati mahususi na utapitishwa kwenye ngazi mbalimbali za maamuzi serikalini. Tunataka Watanzania wajue serikali inajali watu wake na ipo makini kwa jambo kumbwa kama hili la kuokoa nguvu kazi ya taifa," alisema.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema motisha kwa watumishi imeanza kwa baadhi ya halmashauri kutenga hosteli kwa watumishi wanaotoa huduma wakae kwa siku 14 kabla ya kuungana na familia zao.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Faustine Ndugulile, alisema upotoshaji umekuwa mkubwa kutokana na watu wengi kujigeuza wasemaji na madaktari, akitaka wataalamu kuachwa kufanya kazi ili kupunguza taharuki katika jamii.

# HAALAND: RONALDO NDIO HAMASA YANGU



**DORTMUND,** Ujerumani

STRAIKA wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, amesema nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo ndio mchezaji anayemvutia zaidi.

Haaland amekuwa na msimu wa kuvutia 2019-20, na kujikuta akiwaniwa na miamba wa Hispania, LaLiga, Real Madrid.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 19, amefunga mabao 28 katika mashindano yote msimu huu akiwa na Salzburg kabla ya kujiunga na Dortmund Januari, ambako amefunga mabao mengine 12 katika mechi 11 tu kabla ya mlipuko wa virusi vya corona.

Haaland amesema mshindi mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo, ndio ni mtu aliyemhamasisha.

"Unaweza kuona sura ya Ronaldo na kwamba 'leo mimi ni mtu na leo nitafunga mabao' na hivyo ndivyo anavyofanya," amesema Haaland akiiambia ESPN, kwamba alikuwa akimwangalia Ronaldo wakati akikua.

"Yeye ndio amekuwa mfano wangu, amenifanya niwe na njaa ya mafanikio na kutaka kuwa kama yeye.

"Nilikuwa nikimwangalia tangu nakua na nilikuwa naamini siku moja nitakuja kuwa kama yeye, ingawa bado kabisa sijafikia mafanikio yake, lakini yeye ndiye hamasa yangu."

# Totti amtaka Tonali kuwa kama Gerrard

**ROME,** Italia

FRANCESCO Totti, amemtaka Sandro Tonali kupambana na kuwa mmoja wa viungo bora duniani sawa na Steven Gerrard, Frank Lampard au Daniele De Rossi.

Kiungo huyo wa Brescia, Tonali, mwenye umri wa miaka 19, amekuwa akihusishwa na kutakiwa na klabu kubwa Ulaya, akiwa ameanza kuichezea timu ya taifa ya Italia mwaka jana.

Klabu za Barcelona, Juventus, Inter Milan na AC Milan zimeripotiwa kumwania kiungo huyo, ambaye amekuwa akifananishwa na gwiji wa Italia, Andrea Pirlo.

Totti, gwiji wa Italia na AS Roma, anaamini Tonali atajiimarisha kama mmoja wa viungo bora duniani.

"Atakuwa mmoja wa viungo bora kabisa wa kati duniani, kama Gerrard, De Rossi au Lampard," alisema akimwambia mtangazaji wa televisheni, Paolo Bonolis wakati wa mahojiano live kupitia Instagram.

"Staili yake ya uchezaji ni sawa na muunganiko wa watu wawili Pirlo na (Gennaro) Gattuso. Ana kila kitu ambacho mchezaji anatakiwa kuwa nacho."

"Ana uwezo mkubwa wa kubadilisha mchezo, fundi na mbunifu ambaye mara zote akiwa uwanjani anakuwa ametulia, mechi zote muhimu anazifanya kuwa rahisi."





# *Ibrahimovic alinganishwa na Roger Federer*

**MILAN,** Italia

KOCHA wa AC Milan, Stefano Pioli, amemlinganisha mshambuliaji Zlatan Ibrahimovic na gwiji wa tenisi, Roger Federer.

Ibrahimovic ameonyesha kiwango cha kuvutia tangu alipojiunga tena na Milan Januari kabla ya msimu wa Serie A kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Mshindi huyo wa mataji akiwa na Milan, Inter, Barcelona, Paris Saint-Germain, Manchester United na Ajax, Ibrahimovic amefunga mabao manne katika mashindano yote katika kipindi chake cha pili kucheza pale San Siro akiwasili kutoka LA Galaxy ya Marekani.

Wakati majaliwa ya Ibrahimovic kuendelea kucheza hapo Milan yakiwa shakani ambapo alisaini mkataba wa awali hadi mwishoni mwa msimu, Pioli amemlinganisha nyota huyo mwenye umri wa miaka 38 na mshindi mara 20 wa grand slam, Federer.

"Nimezungumza nae, yuko vizuri," amesema Pioli wakati wa mahojiano live kupitia Instagram. "Nafikiri kipaji chake kina ubora wa hali ya juu na sio jambo gumu kwangu kuona kiwango chake.

"Namuona kama Roger Federer, ambaye amezaliwa na kipiaji, lakini amekuwa akifanya kila kitu kuhakikisha anakuwa bora kila siku."

# Sancho atakiwa kutua Liver

**LIVERPOOL,** England

TRENT Alexander-Arnold, angependa Jadon Sancho kujiunga na Liverpool, akimsifia nyota huyo wa Borussia Dortmund kama ni mtu mwenye kipaji cha pekee.

Sancho mwenye umri wa miaka 20, amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Ligi Kuu England, ingawa Manchester United wameripotiwa kwamba wapo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili nyota huyo wa Timu ya Taifa ya England. Lakini mchezaji mwenzake wa England, Alexander-Arnold, angependa kucheza pamoja na Sancho, ambaye alijiunga na Dortmund akitokea Manchester City mwaka 2017.

"Kama akija kwetu, ataifanya timu yetu kuwa bora," amesema beki huyo wa kulia wa Liverpool akimwambia Michael Dapaah wakati wa mahojiano live kupitia mtandao wa kijamii wa Instagram.

"Hivyo, nitakuwa na zaidi ya furaha kucheza na yeye hapa England na ana kijapi cha kipekee, kipekee, kipekee sana."

Sancho alikuwa na kiwango cha kuvutia msimu huu kabla ya ligi kusimamishwa Machi, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Mshambuliaji huyo amefunga mabao 14 na kutoa asisti 15 katika mechi 23 za Bundesliga wakati msimu uliposimamishwa.






# ARSENAL YAJITOSA KUMSAJILI FEKIR

**LONDON,** England

ARSENAL inaendelea kusaka wachezaji kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake huku mmoja wa nyota wanayemwinda, Nabil Fekir, ameiambia Real Betis anataka kubakia katika klabu hiyo.

Kiungo huyo mchezeshaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa amekuwa katika kiwango kizuri msimu huu kabla ya kusimama kwa LaLiga kutokana na kujikinga na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona.

The Gunners na AC Milan zinahusishwa kuanza mchakato wa kumwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 lakini Fekir ameweka wazi anataka kuona anaendelea kuitumikia Betis, gazeti la Marca limeandika.

Fekir aliendelea kusema atakuwa tayari kuondoka hapo na kujiunga na vigogo Real Madrid au Barcelona au kama Betis itaamua kumhamisha kutokana na matatizo ya fedha yaliyosababishwa na madhara ya Covid-19. Kiungo huyo amesababisha klabu yake kufanya vizuri kwenye ligi hiyo ya juu Hispania, akiwa amefunga mabao saba na kutoa pasi za mwisho sita kwenye michezo 23 aliyocheza.

Mwaka 2018, Fekir alikaribia kujiunga na Liverpool akitokea Lyon inayoshiriki Ligue 1 lakini uhamisho wake uliokwama katika dakika za lala salama.

Kutokana na kuwindwa na klabu hiyo ya Merseyside pamoja na Arsenal, Fekir alisaini mkataba wa miaka minne wa kuitumikia Betis ambao una thamani ya pauni milioni 22 Julai mwaka jana.

# *Upatina wa Martinez, Messi utavutia wachezaji - Kocha*

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Quique Setien, amemzungumzia mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez na kusema akicheza pamoja na Lionel Messi itakuwa "hamasa kubwa" kwa wachezaji.

Martinez amekuwa akihusishwa sana na uhamisho wa kwenda kwa miamba hao wa LaLiga, ambao pia wameripotiwa kumwania nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 tayari anacheza pamoja na Messi kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Argentina, na amefunga mabao tisa katika mechi 17 alizoichezea.

Alipoulizwa kuhusu Martinez, Setien alisifia kipaji cha fowadi huyo - na kusema kucheza pamoja na Messi kunaweza kuvutia wachezaji wengi zaidi kujiunga na Barcelona.

"Lautaro Martinez ni mchezaji wa kiwango cha juu," amesema Setien akiliambia gazeti la La Gazzetta dello Sport.

"Messi anampenda? Tunatakiwa kumuuliza. Wachezaji wote wazuri wanaweza kuvutiwa na kutakiwa Barcelona. "Kutokana na ukweli kwamba wengi wangependa kucheza na Leo na ujio wa Martinez itakuwa hamasa kubwa."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# AGUERO: WACHEZAJI WANAHOFIA CORONA

Wanaogopa Ligi Kuu England ikirejea wanaweza kuziambukiza familia zao...

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester City, Sergio Aguero, anaamini wachezaji wengi "wanaogopa" kurudi uwanjani kuendelea na Ligi Kuu England baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

Ripoti zinasema kwamba, Ligi Kuu England inaweza kurudi mwanzoni mwa Juni baada ya kusimamishwa Machi mwaka huu, huku mkutano wa kuamua hilo ulitarajiwa kufanyika jana Ijumaa.

Lakini Aguero anahisi kwamba wachezaji wengi wanahofia ugonjwa wa COVID-19, ambao umeripotiwa kuua watu zaidi ya 233,000 duniani kote.

> **"Wachezaji wengi wanaogopa kwa sababu wana familia, wana watoto, na vichanga," amesema akiiambia televisheni El Chiringuito.**

"Wakati tutakaporudi, nafikiri kwamba kutakuwa na hofu kubwa, tutakuwa makini sana na wengi wao wanaogopa, 'nini kitatokea pale?'

Uingereza kwa upande wake janga hili la virusi vya corona limesababisha watu zaidi ya 171,000 kuambukizwa na vifo kufikia 26,000.

Nyota huyo wa Argentina, Aguero amesema wachezaji wengi watarudi uwanjani huku wakiwa hawajiamini kabisa.

"Ninaogopa, lakini nipo na mpenzi wangu hapa na nitawasiliana na watu wengine. Nimejifungia nyumbani na mimi ndio pekee naweza kumuambukiza mpenzi wangu," amesema Aguero.

"Wanasema kwamba kuna watu wana maambukizi, lakini hawaonyeshi dalili zozote na bado wanaweza kuwaambukiza wengine. Ndio maana nipo hapa nyumbani."

## ZISIKUPITE

### GREALISH AKARIBIA UNITED

MANCHESTER United imeamua kuendelea na mchakato wa kumsajili kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish (24), badala ya nyota mwenzake katika kikosi cha Timu ya Taifa ya England na Leicester, James Maddison, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Manchester Evening News)***

### MADRID, BARCA VITANI

REAL Madrid na Barcelona zimeingia katika vita ya kuwania saini ya winga wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, anawaniwa pia na Manchester United. ***(Bild - in German)***

### FEKIR AGOMBEWA ULAYA

ARSENAL itakutana na ushindani kutoka kwa AC Milan katika kumsajili kiungo wa Real Betis na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Nabil Fekir, ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Marca - in Spanish)***

### BAYERN YATENGA DAU

BAYERN Munich imesema iko tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 60 tu kwa ajili ya kufanikisha mchakato wa kumsajili winga wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Leroy Sane (24). ***(Sky Sports)***

### BEI YA COUTINHO YATAJWA

BARCELONA imeweka wazi haitakuwa tayari kumuuza winga wa Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho chini ya dau la pauni milioni 87. Chelsea inahusishwa na mipango ya kumwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### MOSES ATAKIWA MILAN

INTER Milan inajiandaa kumsajili kwa mkopo Victor Moses (29), na baadaye kumpa mkataba wa kudumu lakini inaitaka Chelsea iondoe ada ya pauni milioni 10 ambazo imeweka ili kumtoa winga huyo wa Timu ya Taifa ya Nigeria. ***(Calciomercato)***

### BARCA, CITY WATETA

MANCHESTER City imeanza mazungumzo na Barcelona kwa ajili ya kunasa saini ya beki wa kulia wa Ureno, Nelson Semedo (26). Mchakato wa usajili huo utamhusisha pia beki wa kulia, Joao Cancelo (25), ambaye ataenda katika klabu hiyo ya England. ***(Sport)***

### FERNANDINHO KUULA

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Brazil, Fernandinho, ambaye ana umri wa miaka 34, anataka kusaini mkataba mpya na klabu yake ya Manchester City. ***(Sky Sports)***

### FRASER KUTUA SPURS

WINGA wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Scotland, Ryan Fraser, ambaye ana umri wa miaka 26, anataka kujiunga na Tottenham mara mkataba wake utakapomalizika katika majira ya kipindi cha joto. ***(Football Insider)***

### ARSENAL YATOA MSIMAMO

MKUU wa Kitengo cha Soka cha Arsenal, Raul Sanllehi, amewaambia wafanyakazi wa klabu hiyo kuwa suala la usajili wa wachezaji sio kipaumbele chao katika kipindi kinachokuja cha majira ya joto. ***(Standard)]***

HABARI MICHEZO

## Mlandege yaeleza kilio cha timu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Mlandege FC, Mbaraka Himid, amesema timu zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar zinaendelea kupata hasara ya kuwalipa mishahara wachezaji wake bila ya kuwapo kwa mechi za ligi kama walivyokubaliana.

Ligi Kuu Zanzibar imesimama sambamba na ligi nyingine mbalimbali duniani kwa sababu ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona (COVID 19).

Himid aliliambia gazeti hili msimu huu umekuwa na changamoto mbalimbali na klabu zimeendelea kutumia kiasi kikubwa cha fedha kuhudumia timu.

Kiongozi huyo alisema Mlandege wanaendelea kulipa mishahara ya wachezaji kwa mujibu wa mikataba yao bila ya kufahamu hatima ya ligi hiyo ambayo hutoa mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Klabu zinatumia gharama kubwa za kuwalipa mishahara wachezaji huku hakuna mechi yoyote ya ligi inayochezwa, kiubinadamu huwezi kumnyima mshahara kwa sababu ni haki yake kupata kwa mujibu wa mkataba wake mliokubaliana, lakini hatujui kama itaendelea au itafutwa, hasa ukizingatia ligi yenyewe haina mdhamini," Himid alisema.

Aliongeza kabla ligi hiyo haijasimama, timu yao ilikuwa inafanya vizuri na iliweka mipango ya kuhakikisha inamaliza msimu katika nafasi tatu za juu.

## Ihefu yajipanga kusajili chipukizi

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Ihefu FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza umesema usajili wao utazingatia zaidi kuwapa nafasi wachezaji vijana wenye vipaji ili lengo lao la kuendeleza soka hapa nchini litimie, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Ihefu FC, Fred Chalamila, alisema ili malengo ya kuendeleza na kukuza soka nchini yatimie, ni lazima kuwapa nafasi wachezaji chipukizi waonyeshe vipaji vyao.

Chalamila alisema bado malengo yao ni kupambana kuhakikisha wanapata nafasi ya kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Tunahitaji kucheza Ligi Kuu, pia tunaangalia malengo yetu kwamba mbali na kushiriki bali tuwe na vijana wenye umri mdogo kwa ajili ya kuwaendeleza poa kufanya biashara katika Soka," alisema Fred.

Kiongozi huyo alisema mbali na kikosi chao cha kwanza kinachoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, pia wanazihudumia vema timu zao mbili za vijana za umri chini ya miaka 20 ( U-20) na ya (U-17).

Katika msimamo wa Ligi Daraja la Kwanza Kundi B, Ihefu iko katika nafasi ya pili wakilingana pointi na Dodoma FC, lakini wakizidiwa idadi ya mabao ya kufunga na klabu hiyo.

# MAPUMZIKO YA CORONA YAINUFAISHA NDANDA FC

**Na Saada Akida**

LICHA ya hatima ya msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2019/20 kutofahamika hadi sasa kutokana na kujikinga na ugonjwa wa corona, Kocha Mkuu wa Ndanda FC ya Mtwara, Abdul Mingange, amesema wachezaji wake waliokuwa majeruhi wanaimarika na kwake imekuwa ni neema.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mingange alisema kwa upande wake uamuzi wa kusimamisha ligi umekuwa na faida kwa sababu baada ya kurejea tena ligi hiyo, nyota waliokuwa majeruhi watakuwa wamepona na tayari kuisaidia timu.

**Mingange alisema wachezaji wake waliokuwa majeruhi, sasa wameanza mazoezi mepesi na anaamini watakuwa fiti kumaliza mechi zilizosalia za msimu huu.**

"Bado hatujui ni lini ligi yetu itarejea, ila kipindi hiki kinawafanya nyota wangu waliokuwa majeruhi kurejea katika ubora wao, wamepona na wataongeza nguvu kwenye kikosi," alisema Mingange.

Aliongeza kuwa tayari makocha waliokuwa kwenye sintofahamu, sasa hali hiyo imeondoka na watakaporejea uwanjani, watarudi na vikosi kamili.

"Huu ni muda kwa wachezaji wetu waliotoka katika majeruhi kutumia vizuri kwa ajili ya kujifua, hakuna muda wa kupoteza endapo ligi itarejea, nina imani hakutakuwa na muda wa kupoteza kuanza upya katika maandalizi," alisema Mingange.

Kocha huyo alisema amekuwa mkali kwa nyota wake kwa sababu anataka kuhakikisha kila mchezaji anakuwa makini na kuacha kubweteka kuona muda mzuri wa kupumzika na kusahau majukumu yao.

Ndanda FC yenye pointi 31, katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara iko nafasi ya 16 baada ya kushuka dimbani mara 29 huku Singida United inayoburuza mkia ina pointi 15.



Golikipa wa Azam FC, Razak Abalora, ambaye ni raia wa Ghana, akifanya mazoezi ili kuimarisha kiwango chake kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam kabla ya Ligi Kuu Bara haijasimama kupisha maambukizi ya ugonjwa wa corona. **PICHA: JUMANNE JUMA**



# *Bosi Mburahati Queens afariki*

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Soka cha Wanawake Dar es Salaam (DWFA), na mmiliki wa timu ya Mburahati Queens, Dk. Maneno Tamba, amefariki dunia jana mchana, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Wanawake Tanzania (TWFA), Amina Karuma, alisema chama chake kimepokea taarifa za kifo cha mdau huyo kwa mshtuko na masikitiko makubwa.

Karuma alisema Dk. Tamba alikuwa ni 'kiungo' na mshauri muhimu katika kuendeleza gurudumu la soka la wanawake hapa nchini na kifo chake kimeacha pengo katika mchezo huo.

"Sina la kusema, ni kweli Dk. Tamba amefariki, unajua alivyokuwa mtu muhimu sana kwetu (TWFA), huwezi kuzungumzia historia ya soka la wanawake Tanzania bila kumtaja mwenyekiti wetu, tumepoteza mtu muhimu sana," alisema Karuma.

Kocha Msaidizi wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Edna Lema, aliliambia gazeti hili mafanikio yake katika soka yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na Tamba ambaye alikuwa akiwalea wachezaji kama watoto wake.

"Alikuwa ni mzazi, alitusaidia ndani na nje ya uwanja, tumepoteza mdau muhimu katika mapambano yetu, kila siku alitamani kuona tunafanya vizuri," alisema Lema.

Michezo
Jumamosi Mei 2, 2020
Nipashe



Aguero: Wachezaji wanahofia Corona

UKURASA 22



Mashabiki wa Klabu ya Yanga, wakishangilia baada ya timu yao kuibuka na ushindi wa bao 1-0, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa Machi 8, mwaka huu. **PICHA: MAKTABA**

# Dk. Reginald Mengi: Mwasisi wa klabu kujiendesha kisasa

## ●●● Yanga yakubali kuyafanyia kazi ikiwa imepita miaka 26, huku watani zao Simba tayari wameanza...

**Na Adam Fungamwango**

Dk. Reginald Mengi, alipeleka mawazo yake klabu ya Yanga kutaka klabu hiyo ibadilike na kujiendesha kama kampuni. Hiyo ilikuwa ni mwaka 1994, ikiwa chini ya George Mpondela 'Castro' (marehemu).

**Dk. Mengi alipeleka mapendekezo hayo, baada ya wafanyabiashara waliokuwa wakiifadhili klabu hiyo huko nyuma, Mohamed Viran, Abass Gulamali na Murtaza Dewji kila mmoja kwa wakati wake kujiweka kando.**

Mpondela alisimama kidete kutaka mabadiliko ya klabu kuwa kampuni ambayo yalikuwa na baraka za Dk. Mengi, lakini baadhi ya wanachama wa Yanga waliokuwa wakiitumia klabu hiyo kujinufaisha na kwa kuhofia kesho yao, waliligomea katakata wazo hilo na kusababisha Mpondela kujiuzulu.

Kama wanachama wa Yanga wakati huo wangesikiliza na kutekeleza mapendekezo ya Dk. Mengi (pichani), Yanga ingekuwa klabu ya kwanza Afrika Mashariki kuingia kwenye mfumo wa uendeshaji wa kisasa na leo hii ingekuwa na mafanikio makubwa ndani ya uwanja, ikiwa na wachezaji wazuri na gharama kubwa, na nje ikiwa na uchumi imara usioyumba.

Ingekuwa inatimiza miaka 26 tangu iwe kampuni, hivyo ingekua mbali sana na huenda ingekuwa imeshatwaa hata Kombe la Afrika, kama si kuingia robo fainali au fainali ya michuano hiyo.

Matokeo yake leo hii tunaona watani zao Simba ikiwa timu ya kwanza Afrika Mashariki kubadilisha mfumo wa uendeshaji kwa kumpa mfanyabiashara, Mohamed Dewji 'MOO', hisa za asilimia 49.

Kwa muda mfupi tu tangu aingie, tayari Simba imeshacheza robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Miaka michache tu baadaye baada ya mafanikio ya watani zao, wanachama na mashabiki wa Yanga wakakumbuka maneno na mapendekezo ya Dk.Mengi, na sasa wamerejea kule kule kwa kutaka mfumo ubadilike.

Ni wakati huo wa mgogoro mkubwa chini ya Mwenyekiti Rashid Ngozoma Matunda, Yanga ilikuwa inapitia kwenye kipindi kigumu kuliko ilichokuwa nacho hata msimu uliopita chini ya Kocha Mwinyi Zahera, kiasi cha kushindwa hata kuisafirisha timu kwenda Afrika Kusini kucheza mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.



Dk. Mengi aliingia kati na kuokoa jahazi ili timu iende na kucheza mechi za kimataifa, pamoja na za ndani pia.

Pamoja na hayo, Dk. Mengi alifanya utafiti na kugundua tatizo, hivyo akashauri kuwa ili kutibu tatizo la 'njaa' ya mara kwa mara klabu ikubali kuendeshwa katika mfumo wa kampuni, wazo lililoungwa mkono na Mpondela.

Kwenye klabu za Simba na Yanga, kuna baadhi ya wanachama ambao wako kimaslahi na wengine ni wahafidhina tu wasiotaka mabadiliko.

Na wakati huo jambo kama hilo lilionekana ni geni kwa klabu za Tanzania ambazo hadi leo bado zinajiendesha kwa mfumo wa kizamani wa kutegemea ada za wanachama ambazo ni kidogo, hivyo baadhi yao walilipinga kwa nguvu zote.

Mapema mwaka 2000, Abass Tarimba alirejea tena na wazo la Dk. Mengi, lakini naye alikumbana na upinzani kutoka kwa Yusuph Mzimba na kundi lake, hapo ndipo yalipozaliwa makundi ya Yanga Asili na Yanga Kampuni yaliyokuwa na mgogoro uliodumu kwa muda mrefu.

Dk. Mengi, kwa mara nyingine alijitosa tena kusuluhisha mgogoro huo, lakini pia akitumia fursa hiyo kuwapa elimu ya kwa nini Yanga ilipaswa kuwa kampuni.

Inawezekana wakati huo wengi hawakumwelewa. Wazo lake limekaa miaka 26 na sasa Wanayanga wameshaelewa nini baada ya mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji wa klabu na wameshadhamiria kwenda huko.

Wakati Yanga wako mbioni sasa kwenda kwenye mabadiliko, wasisahau kumpa heshima yake muasisi wa mapendekezo hayo ndani ya klabu hiyo ikiwa imepita miaka 26, na sasa ndiyo yameanza kufanyiwa kazi.

Dk. Mengi atakumbukwa daima kwenye tasnia ya michezo si kwa kufanya hivyo upande wa Yanga tu. La hasha.Wazo lake hilo ndilo lililofanyiwa kazi na Simba ambayo kwa sasa inaendeshwa kama kampuni.

Atakumbukwa kama ndiyo mwasisi mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji wa soka kisasa kwenye historia ya mpira wa Tanzania.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >